MSIMBO WA MODULI: CCMKK401 - KISWAHILI KATIKA SEKTA TOFAUTI ZA KAZI

DARAJA LA NNE

MWAKA WA MASOMO: 2020

KITENGO CHA KWANZA: KUTUMIA KIMAZUNGUMZO ISTILAHI ZINAZOHUSIANA NA KAZI

1.1 Mazungumzo kuhusu kujieleza/kujitambulisha

Mutoni: Habari za asubuhi?

Sam: Ni nzuri, habari zako?

Mutoni: Nami ni nzuri

Sam: Vizuri. Je, unaitwa nani?

Mutoni: Ninaitwa Mutoni wewe unaitwa nani?

Sam: Ninaitwa Sam, unaishi wapi?

Mutoni: Ninaishi nchini Rwanda, Jimbo la / mkoa wa Kaskazini, wilaya ya Musanze, Tarafa/sekta ya Muhoza, Kata/seli ya Mpenge, kijiji/kitongiji cha Giramahoro. Wewe unaishi wapi?

Sam: Na mimi ni hapo, niko jirani yako. ndipo ulizaliwa?

Mutoni: Hapana nilizaliwa Jijini Kigali nipo hapa kwa sababu ya masomo. Ninasomea kwenye **IPRC KIGALI**. Wewe vipi?

Sam: Nami sikuzaliwa hapa, nilizaliwa katika wilaya ya Muhanga. Nipo hapa kwa sababu ya kazi, niko makanika kwenye banda la motokaa (gereji) mjini Musanze.

Mutoni: Sawa tutaonana baadaye.

Sam: Kwa heri ya kuonana

Mutoni: Kwa heri

Maneno ya kuzingatia: *Jina, Nchi, Jimbo, Wilaya, Tarafa, Kata, Kijiji/Kitongoji, unaishi wapi?, ulizaliwa wapi? banda la motokaa*

Zoezi

Husisha maneno kwenye safu ya **A** na maana yake kwenye safu ya **B**

A	B
Kijiji	District
Wilaya	Where were you born?
Unaishi wapi?	Garage
Ulizaliwa wapi?	Country
Nchi	Village
Banda la motokaa	Where do you live?

Kazi ya nyumbani (katika makundi ya watu wawili wawili)

Andika mazungumzo kati ya watu wawili wakiulizana na kujibizana juu ya utambulisho.
Tanbihi: Katika mazungumzo yako usikose kuuliza **jina, mahali anapoishi, mahali alipozaliwa, hali yake ya ndoa na** mwishowe **swali kuhusu kazi yake.**

Kiwanda

Kiwanda ni mahali ambapo bidhaa mbalimbali hutengenezwa, yaani penye majengo na mashine. Bidhaa hizo zinaweza kuwa ndoo, sahani, mabakuli, vijiko, masufuria, magari, kompyuta, bati, vyakula mbalimbali, nyundo, pasi, baiskeli, pikipiki na vitu mbalimbali kwa ujumla. Hivyo kuna aina mbalimbali za viwanda: vipo viwanda vya vyakula, vya magari, vya vifaa vya ujenzi, vya vyombo mbalimbali, na vya vitu vizito, vya vyuma n.k.

Faida na hasara

Kila nchi ina viwanda mbalimbali. Viwanda hivyo huisaidia nchi hiyo pindi iuzapo bidhaa hizo, pia huisaidia nchi husika kunufaika kiuchumi kwa uwepo wa viwanda hivyo. Viwanda vina faida kubwa sana katika nchi yenye viwanda hivyo; faida hizo ni: Kuisaidia nchi kukua kiuchumi, kupata fedha za kigeni, kulipa madeni wanayodaiwa, kuajiri watu ambao hawana kazi, na kunufaisha taifa kwa ujumla n.k.

Tunapokuwa na viwanda tunanufaika kwa vitu vingi. Lakini viwanda vina madhara pia, tena mengi sana. Madhara hayo ni: Moshi unaotoka viwandani huharibu anga hewa (ozon layer) ambapo anga linapotoboka husababisha kuwa na joto kali sana, Majitaka yanayotiririshwa kwenye mito husababisha madhara kwa viumbehai wa majini na watu wanaotumia maji ya mto huo, Uchafu unaobaki husababisha magonjwa mbalimbali ya milipuko, Miwanda hutoa hewa chafu ambayo husababisha matatizo ya upumuaji kwa ujumla. Kwa hiyo tuvitunze viwanda vyetu ili vilete faida, si kuangamiza watu na viumbe wengine.

Kampuni ya Ujenzi

Ujenzi ni teknolojia ya kujenga nyumba, viwanda, barabara, daraja au hata miji. Ujenzi ni kazi inayohusisha watu wengi na ngazi mbalimbali ya kupanga na kutekeleza. Majengo madogo yajengwa na watu wenyewe kufuatana na maarifa yao bila mpangilio mkubwa. Wajenzi hutumia maarifa ya watu waliowatangulia. Majengo makubwa zaidi huhitaji mpangilio mwangalifu. Mwenye jengo atatafuta kwanza ushauri wa wataalamu. Msanifu atachora ramani. Wataalamu wengine hukadiria mahitaji ya vifaa na gharama za jengo. Vibali vinahitajika.

Wajenzi watakaa na kupanga mahitaji ya muda, pesa, wafanyakazi na mashine. Wahandisi na mafundi wa fani mbalimbali hushirikiana.

Uongozi wa kampuni ya ujenzi

- Chief Executive Officer (President): Mkurugenzi mkuu
- Project Manager: Meneja wa mradi
- Civil Engineer: Mhandisi
- Structural Engineer: Mhandisi wa miundo
- Quantity Surveyor: Mchunguzi wa wingi
- Land Surveyor: Mchunguzi wa ardhi
- Company's Lawyer /: Mwanasheria wa kampuni
- Admin and HR Manager: Meneja wa rasilimali.
- Business Developer: Mwendelezaji wa biasharara
- Accountant: Mhasibu
- Secretary: Katibu/ mpokezi.

KAZI (AMALI) ZA UFUNDI MBALIMBALI

- Maana ya neno kazi au amali ni shughuli anayofanya mtu binafsi au kundi fulani k.v. kulima, kuandika, kufundisha, n.k.
- Kama tunavyojua ulimwenguni, watu hufanya kazi mbalimbali. Baadhi ya kazi hizo zinazofanywa, huweza kufanywa kwa kutumia mikono na nyingine zikafanywa kwa namna nyingine.
- Kuna amali au kazi za kisayansi ambazo ni za hali ya juu. Na kuna nyingine ambazo ni za chini na wastani. Hizi hazihitaji utaalamu mwingi. Kazi zile zifanywazo kwa kutumia mikono, huweza kufanywa na yeyote mzima tu na mwenye nguvu. Isipokuwa kazi za kisayansi, kuna pia kazi za kienyeji. Katika kazi za kisayansi tunaweza kutoa mfano k.v. udaktari, ualimu, utangazaji, n.k.
- Kwa kawaida mtu akiwa mgonjwa, huhitaji apelekwe hospitalini pale ambapo atakutana na daktari ambaye ujuzi wake ni mkubwa zaidi kuliko wengine.
- Kadhalika, mgonjwa akiwa mtamaduni sana, huo huhitaji matibabu ya kienyeji. Kwa hiyo huyu hupelekwa kwa mganga wa kienyeji; na kazi hiyo itakuwa kazi ya kienyeji. Waganga hawa nao huwa katika aina tofauti tofauti. Kuna yule wa **kutazamia** tu, na yule wa **kutibu**. Yule wa kutazamia ni mchunguzi tu, yaani anachunguza kisha akakuelezea kasoro tu. Lakini yule wa kutibu anachunguza na kugundua kasoro kisha akampa mgonjwa matibabu. Wapo waganga wengine wa kutia ulozi na wengine wa kutoa ulozi huo.
- Zipo kazi nyingine kama vile **ualimu, uanasheria, uanasayansi, umakanika, ushonaji, umalenga, uokaji, ususi, usonara, ubawabu, usogora, unajimu, udobi, ulimaji au ukulima, unyozi, uchuuzi au uuzaji, ufinyanzi, uhasibu, uhudumu, uanajeshi, utangazaji, useremala, upishi, uuguzi, n.k.**
- **Mwalimu** kazi yake ni kufunza, lakini **mwanasheria** huwatetea wateja wake koritini. Naye **mwanasayansi** hufanya utafiti wa kisayansi. Lakini **makanika** hurekebisha magari yaliyo na

hitilafu. **Mshonaji** naye hushona na kurekebisha nguo za watu. Naye **malenga** ni mtunzi wa mashairi, yaani hufanya kazi ya kutunga mashairi; tunaweza kumwita pia **mshairi.**

- **Mwokaji** na **msusi** hufanya kazi tofauti tofauti. Mwokaji yaweza kuwa ni **mtengenezaji** wa mikate ama mchoma nyama au mahindi. **Msusi** husuka nywele tu. **Sonara** ni fundi wa kutengeneza vitu vya mapambo kama vile pete, mikufi, n.k. Lakini **sogora** ni fundi wa kucheza ngoma.
- **Mnajimu** ni mtu mwenye elimu ya kutabiri utokeaji wa matukio hasa hasa kulingana na elimu ya nyota. Kazi ya **ubawabu** hufanywa na **Bawabu** ambaye ni mlinda lango. Naye **dobi** ni mtu afanyaye kazi ya kuwafulia watu nguo na kisha kuzipiga pasi ama kwa mkono au kwa mashine.
- Zipo kazi nyingine nyingi pamoja na wafanyakazi wake. Kwa mfano kuna **mshenga, mhunzi, balozi, hakimu, mzegazega, mkalimani, sarahangi, dalali, n.k.**
- Kazi kubwa ya **dalali** ni kunadi vitu mnadani na kumuuzia aliye na pesa nyingi zaidi. **Sarahangi** ni mdogo au naibu wa nahodha ambaye hufanya kazi ya nahodha na kuwaangalia mabaharia wakati ambapo nahodha hayupo. Naye **mkalimani** kazi yake ni kufasiri maneno na kuyatafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine.
- **Mzegazega** kazi yake ni uchukuzi wa mizigo hasa maji. Lakini mchuuzi kazi yake ni kuuza vitu kwa rejareja. Na **ubalozi** ni kazi inayofanywa na **balozi** ambaye kazi yake ni kuwakilisha au kusimamia nchi yake katika nchi nyingine. Kuna pia kazi ya **uhunzi** inayofanywa na **mhunzi** ambaye kazi yake ni kufua vyombo vya aina ya vyuma k.v. mishale, majembe, visu, n.k. **Hakimu** naye ni mfanyakazi maalumu, na kazi yenyewe ni kusikiliza na kufuata kesi mahakamani(koritini) na kutoa uamuzi wake.
- Kadhalika, **mshenga** ni mtu atumwaye kwa upande wa mchumba kupeleka posa. Yaani ni mtu atumwaye na mchumba kuwasilisha ujumbe kwa mchumba Yule. Tunaweza pia kusema kazi ya **unyozi** inayofanywa na **kinyozi,** ambaye kazi yake ni kunyoa watu nywele kichwani. Lakini mtu anayefanya kazi ya ufundi wa kujenga nyumba kwa mawe au matofali huitwa **mwashi.**
- Halafu, kuna pia kazi ya **ujasusi** ifanywayo na **jasusi** ambaye hufanya kazi ya upelelezi nje ya nchi yake na kuitafutia habari. Naye **mpelelezi** hufanya kazi ya kuchunguza watu au wahalifu na kutafutia habari nchi yake hasa hasa nchini humo.
- **Tarishi** na **kibarua** ni wafanyakazi tofauti. **Tarishi** ni mhudumu wa ofisi anayetumwa kupeleka barua au habari. Huyu yaweza pia kuitwa **mjumbe, katikiro au mesenja.** Lakini **kibarua** ni mfanykazi wa muda anayeajiriwa kwa hesabu au malipo ya kila siku. Yaweza pia kuwa mfanyakazi wa kimuda. Na yule anayefanya kazi ya kubeba mizigo huitwa **mpagazi.** Huyu anaelekea kuwa kama mzegazega, lakini ikumbukwe kuwa mzegazega anajihusisha sana na uchukuzi wa maji.

- Pengine, tunaweza kusema kazi ya **uuguzi** inayofanywa na **muuguzi** ambaye kazi yake ni kuhudumia wagonjwa. Yaweza pia kuitwa **mualisaji.** Na kazi ya **ufinyanzi** hufanywa na **mfinyanzi** ambaye kazi yake ni kutengeneza vyombo vya udongo kama vyungu, n.k. Kazi ya **uhasibu** ni kazi ifanywayo na **mhasibu** ambaye ni mtaalamu anayehusika uwekaji wa hesabu za pesa. Naye **mhudumu** ni mtu anayefanya kazi ya kutoa huduma kwa watu wengine k.v. kufagia ofisi, kupika chai ya ofisi au kuuza vinywaji kwenye baa. Kazi ya **uanajeshi** ni kazi ifanywayo na wanajeshi au askari ambao kazi yao ni ulinzi wa nchi Fulani**.** Hawa tunaweza kuwalinganisha na wale wanaofanya ulinzi au uchungaji wa usalama wa ndani ya taifa ambao huitwa **askari polisi.** Kazi ya **utangazaji** hufanywa na mtu aitwaye **mtangazaji** ambaye hutangaza na kueneza habari za kitu fulani**. Useremala** ni kazi ifanywayo na **seremala** ambaye ni fundi wa kuranda na kutengeneza samani za mbao au miti. Kazi ya **upishi** ni kazi ifanywayo na **mpishi** ambaye ni mjuzi wa kupika na kutengeneza chakula. **Ulimaji au ukulima** ni kazi inayofanywa na **mlimaji** au **mkulima** ambaye ni mtu anayepata mahitaji yake yote kutokana na jasho lake kwa kulima ardhi anayoimiliki ili aweze kuishi.
- Hali kadhalika, tunaweza pia kuwa na kazi nyingine mbali mbali. Tunaweza kutoa mifano kadhaa k.v. **rubani, muumikaji, mkonokono, mnyapara, yaya, msanii, mcharazi, kocha, mhakiki, mhadhiri, utingo, kondakta au mwangalizi wa abiria.**
- **Rubani** ni mtu anayeendesha na kuongoza ndege. Yaweza pia kuitwa **mwanahewa.** Lakini **utingo** ni mpakiaji na mpakuaji mizigo katika katika chombo k.v. gari. Anaweza kuitwa **taniboi**. **Muumikaji** ni tofauti na **mkonokono. Muumikaji** ni mtu mwenye ujuzi wa kutibu kwa kutoa au kuvuta damu mwilini hasa kwenye sehemu iliyo na maumivu akitumia pembe ya umiko au chuku. Anaweza pia kuitwa **mpiga chuku.** Lakini **mkonokono** ni mganga stadi wa kutibu kienyeji sumu ya nyoka. Naye **mnyapara** ni mtu anayeangalia utekelezaji wa kazi bila yeye mwenyewe kushiriki. Anaweza pia kuitwa **msimamizi** wa kazi. **Yaya** ni mwanamke anayefanya kazi ya kulea na kumtunza mtoto nyumbani.
- **Msanii** ni mtu mwenye ujuzi au ustadi wa kutunga na kutoa mawazo yake kama vile katika mashairi, hadithi, michezo, tamthilia, nyimbo, n.k. kwa kumvuta msanii. Pia yupo **Mcharazi**, yeye hufanya kazi ya kuchapa au kupiga chapa kwa charazi au taipureta. Lakini **kocha** ni mwalimu wa michezo k.v. mpira au riadha. **Mhakiki** ni mtu anayetoa fasiri ya ndani kabisa ya kitu au jambo pamoja na kutoa maoni au fikra zake yake. Naye **mhadhiri** ni mtu anayetoa mhadhara kwa hadhira. Huyu yaweza pia kuwa mwalimu katika chuo kikuu, yaani chuo cha elimu ya juu
- **Dobi** : mtu anayefanya kazi ya kufua nguo na kupiga pasi
- **Mvuvi** :anayefanya kazi ya kuvua samaki

- **Mwokaji** : anayepika mikate
- **Sonara** : anayefua pete na bangili
- **Nahodha** : anayeendesha jahazi
- **Hamali** : anayebeba mizigo bandarani
- **Rubani :** anayeendesha ndege
- **Mtungaji** : anayeandika vitabu
- **Mhariri** : anayechapisha gazeti
- **Mgema** :anayetoa tembo mnazini
- **Mchuuzi** :anyeuza bidhaa zake kwa kuzitembeza
- **Mekanika** :anayetengeneza gari lililoharibika

SEHEMU YA KWANZA: VITAMKWA VYA KISWAHILI NA MSAMIATI WA MSINGI

Lugha ya Kiswahili ina herufi za alfabeti ishirini na nne (24). Herufi hizo zinagawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni irabu (vokali) tano (5). Kundi la pili ni konsonanti kumi na tisa (19).

Alfabeti hizo zote ni hizi zifuatazo: **a,b,c,d,e,f,g,h,i,j,k,l,m,n,o,p,r,s,t,u,v,w,y,z.**

1.1 Irabu au vokali

Irabu za Kiswahili ni tano. Matamshi yake ni kama yale ya lugha ya Kinyarwanda.

Mfano: **a : a**cha, **a**ngalia

e : endelea, **e**mbe

i : ingia, **i**mba

o : ondoka, **o**ndoa, **o**na, **o**rodha

u : ukuta, **u**limi, **u**fagio, **u**dongo, **u**fa, **u**ma, **u**kuta

1.2. Konsonanti

Konsonanti zinazotumiwa katika lugha ya Kiswahili ni kumi na tisa.

Mifano:

b : baba, babu, bibi, bubu

c : herufi hii, haitumiwi peke yake, kila mara hufuatana na «**h**»**.** hivyo hugeuka «**ch**».

Chuchu, chache, chotara, chura, chumba

d : dada, daftari, daktari, dari, debe

f : faida, fahali, faini,faranga, farasi, kifafa

g : goti, godoro, gorofa, gori, gazeti, gereza, goigoi

h : habari, hawara, hawala(cheki,hundi), hekima(akili,busara,ujuzi), herufi,hekalu,homa,hotuba

j : juma, joto, jina, jambazi, jana, jangwa, jela, jua

k : kaka, karamu, kalamu, kazi, katikati, karatasi, kiroboto

l : lazima, labda, lengo, leo, laini, laana, lakini, lisani, lofa, luteni, lusu(mwizi)

m : mama, mwizi, maziwa, mate, miwani, misa, moshi, moto, motokaa,mume

n : nini,nani, noma(kipingamizi), noeli, novemba, nuru

p : pua, papa, pasaka, paredi, pasi, pasipoti, papai,pole

r : ruhusa,rais, roho, rafiki, rajabu, raia,rehema, refa,riziki

s : sisi, samba,sita, sifa,sauti, sasa, soko, safari, sakafu, sufuria, sarufi, sekondari, serikali,sufuri

t : tano,tatu, timu, tembo(ndovu), tabia, takataka, tarafa, tupu, tundu

v : viti, vita, vibaya, vitamini, vokali, visu,vizuri

w : watu, waridi, wao, wakati,wapi, wewe, wilaya, wazazi, wawili,wezi, wimbo, waraka

y : yeye, Yohana, yale, yai, yaya, Yesu, yatima, Yule

z : zeze, zizi, zamani, zahanati, zaidi, ziada, zimwi, zawadi

Isipokuwa irabu na konsonanti, lugha ya Kiswahili huwa na vitamkwa vinavyotokana na mfuatano au muungano wa konsonanti zaidi ya moja. Vitamkwa hivyo ni vifuatavyo:

dh, th, ch, ng', gh, ng, nn, mbw, mch, ny, sh, n.k

Mifano:

dh: fedha, dhambi, dhahabu, dhoruba, dharau, udhaifu, n.k

th: thelathini, themanini, thamani, themometa, theluthi, n.k

ch: chakula, mchezo, chimbuko, chotara, machozi, chura, chache, n.k

ng': kitamkwa hiki huwa na sauti ya pekee inayokaribia kufanana na jinsi tunavyotamka «nk» katika lugha ya Kinyarwanda.

ng'ombe, ng'onzi(kondoo), ng'ambo, ng'ang'ania, n.k

ng: ngozi, ngoma, ngano, nguruwe, ngamia, nguvu, n.k

gh: lugha, gharama, ghasia(fujo), ghala(stoo,bohari), ghadhabu(hasira, hamaki, ghaidhi, mafutu), ghafla, n.k

nn: nne

mbw: mbwa, mbweha(bweha)

mch: mchana, mchaguzi, mchaichai, mchakamchaka, mchoraji, mchumba, n.k

ny: nyanya, nyama, nyani, nyati(mbogo), nyumba, nyuma, nyonyo(chuchu), n.k

sh: shati, shule, shughuli, shuka, shingo, sherehe, shangazi, shemeji, sheria, shetani, shida, n.k.

MAAMKIZI MAAMKUZI, KUSALIMIANA, KUAMKIANA, KUAMKUANA)

SHABAHA ZA SOMO HILI

Baada ya sura hii, kila mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa: 1.Kusalimia na kujibu ifaavyo aina tofauti za maamkizi kulingana na nyakati za siku na jinsi maamkizi hayo yanavyoandikwa. 2. Kuagana na kujibu maagano.

Iwapo tunasalimiana ni lazima tujue ni nani tunayemsalimu au ni nani anayefanya kitendo cha kusalimia. Pia ni lazima tujue kitendo hicho kinafanywa wakati gani au kinafanyiwa wapi? Au mahali kitendo kitendo kinapofanyiwa (mazingira).

NADHARIA YA MAAMKIZI

Tunapozungumzia **"Nadharia ya maamkizi"** huwa tunamaanisha mambo muhimu ya kuzingatia tunaposalimiana.Maamkizi **ni namna ya kujuliana hali**. Kwa hiyo tunapoamkiana tunapaswa kuzingatia mambo matatu yafuatayo:

1. **Majira:** Nyakati za siku au wakati kitendo cha kusalimiana kinapofanywa. Yaweza kuwa **alfajiri**,**macheo,asubuhi,**
2. **Adhuhuri,alasiri,magharibi(machweo), jioni(usiku mchanga)** au **usiku wa manane.**

3. **Mazingira:** Ni vitu na watu vinavyomzunguka mtu mahali alipo. Yaweza kuwa **ofisini, shuleni, kazini, kanisani, msikitini, darasani, shereheni, mazishini, safarini, safarini, n.k**

4. **Rika:** Ni kiwango cha miaka au umri wa miaka ya watu wanaoamkiana.

Iwapo watu wanaosalimiana wako katika rika moja, wanatumia maneno yanayolingana na umri wao. Lakini iwapo wanatofautiana kwa rika au umri wa miaka wanalazimika kuheshimiana kwa kutumia maneno yenyewe.

Kwa mfano: Kama mtu anayesalimia ni mdogo kuliko msalimiwa, analazimika kutumia maneno halisi ya heshima.

Kwa hiyo wanaosalimiana waweza kuwa: **watoto, vijana, watu wakubwa (watu wazima), wazazi, wazee, n.k**

MAAMKIZI DARASANI

Mazungumzo kati ya mwalimu na wanafunzi

Mwalimu anaingia darasani.

Mwalimu: Habari za asubuhi?

Wanafunzi: Nzuri. Shikamoo mwalimu!

Mwalimu: Marahaba! Mimi ni mwalimu. Mimi ni nani?

Kalisa: Wewe ni mwalimu.

Mwalimu: vizuri!

Wewe Kayitesi ni mwanafunzi.

Kayitesi, wewe ni nani?

Kayitesi: Mimi ni mwanafunzi.

Mwalimu: Ninyi wote ni wanafunzi.

Ninyi ni nani?

Wanfunzi: sisi ni wanafunzi.

Mwalimu: Mimi si jambo!

Je, Musafiri wewe hujambo?

Musafiri: Sijambo mwalimu.

Mwalimu: Mimi mzima.

Kalisa wewe mzima?

Kalisa: Mimi mzima.

Mwalimu: Ninyi wote wazima?

Wanafunzi: Sisi wote wazima!

Mwalimu: Vizuri! Kengele inalia kwa heri.

Wanafunzi: Asante mwalimu, kwa heri.

MAAMKUZI NYUMBANI (katika familia)

Mtoto na mama yake

Kayitesi: Hodi hapa!

Mama: Karibu!

Kayitesi: Shikamoo mama.

Mama: Marahaba mtoto wangu!

Kayitesi: Pole kwa kazi mama!

Mama: Asante mwanangu, habari za masomo?

Kayitesi: Ni njema. Habari za mchan wewe?

Mama: Ni nzuri mwanangu, ila kazi inanisumbua!

Kayitesi: Pole sana mama.

Mama: Asante sana mwanangu, nimeishapowa.

Weka vitabu nikutume sokoni.

Kayitesi: Ndiyo mama!

Mama: Nenda sokoni ununue nyama, unga, mchele, viazi, maharage na vitunguu.

Kayitesi: Kilo moja ya mchele ni faranga ngapi?

Mama: Kilo moja ya mchele ni faranga mia mbili na ishirini (220). Je, unaelewa?

Kayitesi: Ndiyo mama!

Mama: Usikawie mwanangu!

Kayitesi: Ndiyo mama, Asante!

Mama: Asante sana mwanangu.

MAAMKIZI MJINI (MITAANI)

Musafiri: Vipi dada?

Umulisa: Salama! Habari za siku nyingi?

Musafiri: Nzuri sana! Je, habari za huku mjini?

Umulisa: Njema Musafiri. Baba na mama hawajambo?

Musafiri: wote hawajambo. Kalisa hajambo?

Umulisa: Hajambo, anakusalimu.

Musafiri: Asante sana! Unakwenda wapi dada?

Umulisa: Ninakwenda sokoni. Nina haraka kidogo.

Musafiri: Vizuri. Kwa heri ya kuonana. Wasalimie nyumbani

Umulisa: Vizuri! Nitawasalimu. Kwa heri.

MAAMKUZI KATI YA WATU WA RIKA MOJA (UMRI SAWA**)**

Kamali na Kakuze

Kamali: Vipi kakuze? Habari za masomo?

Kakuze: Salama. Tunajifunza masomo mapya kama Kiswahili na mengine.

Kamali: Je, masomo mapya yanaeleweka vizuri?

Kakuze: Ndiyo yanasikika kabisa. Habari zako wewe? Unatoka wapi?

Kamali: Mimi niko sawa. Ninatoka mjini kununua vitabu, kalamu, kikapu na viatu.

Kakuze: Sawa kwa heri!

Kamali: Kwa heri ya kuonana!

MAAMKIZI KATI YAWATU WA RIKA AU UMRI TOFAUTI

Mwanafunzi na Mkurugenzi

Kamali: Shikamoo Mkurugenzi!

Mkurugenzi: Marahaba mtoto wangu. Unataka nini?

Kamali: Ninataka shule ili niweze kusomea hapa katika kidato cha nne mkondo wa lugha.

Mkurugenzi: Unatoka shule gani?

Kamali: Ninatoka shule ya Green Hills.

Mkurugenzi: Je, una ripoti ya maksi?

Kamali: Ndiyo Mkurugenzi!

Mkurugenzi: Urudi kesho nitakuonyesha darasa.

Kamali: Asante sana Mkurugenzi!

Mkurugenzi: Safari njema.

NAMNA NYINGINE ZA KUSALIMIANA

- Habari?
- Habari gani?
- Habari za kuamka?
- Habari za tangu jana?
- Habari za tangu juzi?
- Habari za siku nyingi?
- Habari za muda mrefu?
- Habari za miaka?
- Habari za kushinda?
- Habari za usiku?
- Habari za jioni?

MAAMKIZI YA KAZINI

Mteja: Habari za asubuhi?

Mtumishi: Nzuri, shikamoo mteja!

Mteja: Marahaba. Hujambo?

Mtumishi: Sijambo.

Mteja: Mwenzako Nsabimana amelala je?

Mtumishi: Salama.

Mteja:Meneja yuko mzima?

Mtumishi: Mzima.

Mteja: Vizuri sana! Nionyeshe mahali pa kukaa kisha niagize chakula na kinywaji.

MAAMKIZI YA HOTELINI

Mtumishi: Hodi!

Mteja: Karibu.

Mtumishi: Samahani kwa kukusumbua.

Mteja: Si kitu. Habari za asubuhi?

Mtumishi: Njema. Mama shikamoo!

Mama: Marahaba. Habari zako?

Mtumishi: Nzuri. Nimekuja kuangalia ikiwa mnahitaji niwahudumie kitu fulani.

Mama: Asante sana. Bafuni Tunahitaji maji ya moto pamoja na sabuni.

Mtumishi: Ndiyo mama. Hebu niende nikawaletee. Kwa heri. Tutazidi muda mfupi.

Mama: Tutazidi.

MAAMKIZI YA MGAHAWANI

Mtumishi:Vipi dada? Nikusaidie nini?

Mteja: Salama. Habari za kushinda?

Mtumishi: Nzuri. Habari zako?

Mteja: Njema.Wenzako hawajambo?

Mtumishi: Wote hawajambo.

Mteja: Nina lazima ya chakula rojorojo.

Mtumishi: Chakula tu bila nyama?

Mteja : Kuna nyama ya aina gani?

Mtumishi: kuna nyama ya ng'ombe pamoja na ya mbuzi.

Mteja: Sizipendi nyama hizo. Niletee samaki.

Mtumishi: Asante sana, nitawaletea punde sipunde.

TANBIHI: Namna nyingine za maamkizi kwa ujumla.

Maamkizi yenye jibu "**vizuri**","**Salama**"na"**njema**

Habari gani?

Habari za asubuhi?

Habari za mchana?

Habari za usiku?

Habari za kutwa?

Habari za jana?

Tangu jana?

Habari za tangu jana?

Habari za tangu juzi?

Habari za siku mbili?

Habari za muda?

Habari za miaka?

Habari za nyumbani? Habari za Kigali? ....

Umeamka je?

Umelala je?

Umeshinda je? Hali gani?

NAMNA YA KUAGANA

Kwa heri! Haya/Vizuri

Kwa heri ya kuonana!Haya/Vizuri

Tutaonana! Haya/Vizuri

Tutazidi!Haya/Vizuri

Tutaonana baadaye! Haya au Vizuri

Alamsiki(**jioni na usiku**)! Bin-nuru

Mchana mwema! Asante

Usiku mwema! Asante

Ulale salama! Asante

NAMNA YA KUMTAKIA MTU FURAHA / FARAJA NA HUZUNI

1.**FURAHA**: Hongera! Nimehongera/Asante.

Pongezi! Asante.

2. **HUZUNI :** Pole sana! Nishapoa

Makiwa ! Tunayo

2.11 **NAFSI NA VITENZI VYA KIMSINGI**

SHABAHA ZA SOMO HILI

Baada ya sura hii, kila mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa: 1. Kutumia ifaavyo viambishi vya nafsi. 2. 8-Kutumia viambishi nafsi katika mazungumzo ya kawaida.

2.11.1 VIAMBISHI NAFSI HURU

Nafsi	umoja	Wingi
Nafsi ya 1	mimi	Sisi
Nafsi ya 2	wewe	Nynyi/ ninyi/ nyie
Nafsi ya 3	yeye	wao

2.11.2 VIAMBISHI NAFSI AMBATANO

Nafsi	**Umoja**		**Wingi**	
	yakinishi	kanushi	yakinishi	Kanushi
Nafsi ya 1	Mimi ni …	Mimi si…	Sisi tu...	Sisi hatu...
Nafsi ya 2	Wewe u….	Wewe	Nyinyi m...	Nyinyi ham...
Nafsi ya 3	Yeye a….	Yeye ha…	Wao wa...	Wao hawa...

TANBIHI: Katika Kiswahili nafsi zinaweza kutajwa kwa mkato.

Mifano:

1 Wewe na mimi: Wewe nami

2.Nyinyi na sisi: Nyinyi nasi

3. Yeye na wewe: Yeye nawe

4. Wao na nyinyi: Wao nanyi

5. Mimi na wao : Mimi nao

6.Sisi na wao : Sisi nao

SEHEMU YA TATU: SARUFI YA KISWAHILI SANIFU

SHABAHA ZA SOMO HILI

Baada ya sura hii, kila mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa: 1.Kutumia viambishi vya nyakati tofauti katika hali yakinishi na kanushi. 2. Kutumia ifaavyo nyakati tofauti katika mazungumzo ya kawaida. 3. Kukanusha tungo mbalimbali zilizo katika hali yakinishi na kinyume chake. 4.Kutumia Kiswahili Sanifu kutokana na ngeli za Majina

3.1 **MATUMIZI YA NYAKATI**

Wakati, katika Kiswahili huonekana katika vitenzi. Huonyeshwa na viambishi au viwakilishi wakati ndani ya kitenzi. Katika Kiswahili kuna nyakati tano:

i. Wakati uliopo **-na-**
ii. Wakati ujao **-ta-**
iii. Wakati uliopita-**li-**
iv. Wakati wa mazoea-**hu-**
v. Wakati uliotimilika **-me-**

3.1.1 WAKATI ULIOPO (-na-)

Mfano:

Kitenzi kupika

Tungo yakinishi	***Tungo kanushi***
Mimi ninapika chakula	Mimi sipiki chakula
Wewe unapika chakula	Wewe hupiki chakula
yeye anapika chakula	Yeye hapiki chakula
Sisi tunapika chakula	Sisi hatupiki chakula
Nyinyi mnapika chakula	Nyinyi hampiki chakula
Wao wanapika chakula	Wao hawapiki chakula

TANBIHI:

1. Wakati uliopo unatumika kwa kueleza tendo linalotendeka sasa hivi, saa hizi, muda huu. Ni wakati wa sasa.
2. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukuwa Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ na+ kitenzi kilichopoteza(ku).

Mazoezi: weka vitenzi hivi katika wakati uliopo: kujifunza, kucheza, kuzungumza, kulala, kukaa, kucheka, kusema, kushika, kuchukua, kufua, kuchagua,...

3.1. 2 **WAKATI UJAO** (-**TA**-)

Mfano: Kitenzi kupika

Tungo yakinishi	***Tungo kanushi***
Mimi nitapika chakula	Mimi sitapika chakula
Wewe utapika chakula	Wewe hutapika chakula

Yeye a**ta**pika chakula	Yeye hatapika chakula
Sisi tu**ta**pika chakula	Sisi hatutapika chakula
Nyinyi m**ta**pika chakula	Nyinyi hamtapika chakula
Wao wa**ta**pika chakula	Wao hawatapika chakula

TANBIHI:

1. Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vitakavyofanyika wakati utakaokuja baadaye (future tense)
2. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ ta+ kitenzi kilichopoteza(ku).
3. Kufanya mazoezi kuhusu vitenzi: kujifunza kucheza kuzungumza, kulala, kukaa, kucheka, kufua, kuchagua,...

3.1.3. **WAKATI ULIOPITA (-LI-)**

Viambishi wakati katika wakati uliopita ni –**li-** katika hali yakinishi na **-ku-** katika hali ya kukanusha.

Mfano:

Kitenzi:kupika

Tungo ya kinishi	***Tungo kanushi***
Mimi nilipika chakula	Mimi sikupika chakula
Wewe ulipika chakula	Wewe hukupika chakula
Yeye alipika chakula	Yeye hakupika chakula
Sisi tulipika chakula	Sisi hatukupika chakula
Nyinyi mlipika chakula	Nyinyi hamkupika chakula
Wao walipika chakula	Wao hawakupika chakula

TANBIHI:

1 Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vilivyofanyika zamani (past tense)

2 Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukuwa Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ li+ kitenzi kilichopoteza (ku)

3 Kufanya mazoezi kuhusu vitenzi: kujifunza kucheza kuzungumza, kulala, kukaa, kucheka, kufua, kuchagua,...

3.1.4 WAKATI ULIOTIMILIKA (-ME-)

Katika wakati uliotimilika tungo yakinishi, kiambishi wakati ni **-me-.** Katika wakati uliotimilika, tungo kanushi, kiambishi wakati ni **-ja**-.

Mfano: Kitenzi: kufungua

Tungo ya kinishi	***Tungo kanushi***
Mimi ni**me**fungua chupa	Mimi si**ja**fungua chupa
Wewe u**me**fungua chupa	Wewe hu**ja**fungua chupa
Yeye a**me**fungua chupa	Yeye ha**ja**fungua chupa
Sisi tu**me**fungua chupa	Sisi hatu**ja**fungua chupa
Nyinyi m**me**fungua chupa	Nyinyi ham**ja**mefungua chupa
Wao wa**me**fungua chupa	Wao hawa**ja**fungua chupa

TANBIHI:

1.Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukuwa Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ me+ kitenzi kilichopoteza(ku).

3.1.5 **WAKATI WA MAZOEA (HU-)**

Katika wakati wa mazoea, kiambishi **-hu-** huchukua nafasi ya kiambishi nafsi na kiambishi wakati. Wakati wa mazoea humaanisha kutendeka kwa tendo kila siku au kila wakati.Katika kukanusha ni kama vile katika wakati uliopo.

Mfano: Kitenzi kutandika

Hali yakinishi	***Hali kanushi***
Kila siku mimi hutandika kitanda	Kila siku mimi sitandiki kitanda
Kila siku wewe hutandika kitanda	Kila siku wewe hutandiki kitanda
Kila siku yeye hutandika kitanda	Kila siku yeye hatandiki kitanda
Kila siku sisi hutandika kitanda	Kila siku sisi hatutandiki kitanda
Kila siku nyinyi hutandika kitanda	Kila siku nyinyi hamtandiki kitanda
Kila siku wao hutandika kitanda	Kila siku wao hawatandiki kitanda

TANBIHI:

Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukuwa Kiambishi nafsi huru+ hu+ kitenzi kilichopoteza(ku). Hali kanushi ni kama wakati uliopo.

MAZOEZI:

i) Andika tungo hizi katika hali ya kukanusha

a) Wewe utasafisha sufuria.

b) Wewe utafagia darasani.

c) Wewe utakaa juu ya kiti.

d) Yeye alifungua sanduku.

e) Yeye atanawa mikono.

f) Sisi tutapokea wateja wetu

ii) **Andika tungo hizi katika wakati wa mazoea hali yakinishi**

a) Mimi siondoki kazini.

b) Yeye hapiti hapa siku hizi.

c) Wao hawapendi pombe baridi.

iii) Andika tungo hizi katika wakati ujao

a) Polisi alimkamata mwizi.

b) Sisi hutandika vitanda.

c) Wateja wameandika barua mbaya.

iv) Weka tungo hizi katika hali ya kukanusha

d) Mimi nitakunywa chai.

e) Wewe unapenda chakula rojorojo

f) Yeye amenunua chupa mbili..

g) Nyinyi mnatoka kazini.

v) Andika tungo hizi katika hali yakinishi

h) Mukamunana hasafishi sufuria yake.

i) Padiri hajafika hoterini.

j) Mlevi hataanguka njiani.

k) Kamali hakuvaa vizuri

UTUNGAJI WA HABARI KATIKA NYAKATI MBALIMBALI

MIMI NA YOZEFU

Jana mimi na Yozefu tu**li**kwenda sokoni. Sokoni tu**li**nunua vitunguu, chumvi, pilipili, viazi vitamu, maharage na ndizi. Sisi **hu**la viazi na maharage.

Leo asubuhi tu**me**kwenda sokoni tena. Lakini **hatuku**nunua vitu vingi. Leo tu**me**nunua sabuni ya kufulia na sabuni ya kuogea. Sasa mimi ni**na**kwenda dukani kununua sigara na kiberiti. Baba **hu**vuta sigara lakini Mama havuti. Baba **hu**nituma dukani kila siku. Juzi a**li**nituma kununua wembe lakini jana **haku**nituma wembe. Jana Mama a**li**nituma mimi na Yozefu kwenda sokoni.

Kesho mimi na dada tu**ta**kwenda shuleni. **Hatuta**kwenda sokoni wala dukani. Tu**ta**kwenda shuleni kusoma. Tukitoka shuleni tu**ta**rudi upesi nyumbani. Baba yangu ni seremala, na Mama **hu**fanya kazi ya nyumbani. Hivi ni**ta**msaidia Mama kazi za jikoni. Dada **hata**msaidia Baba.

3.2 AINA ZA MANENO

1.Vivumishi

2.Nomino

3.Viunganishi

4.Vihusishi

3.3 NGELI ZA MAJINA

SHABAHA ZA SOMO HILI

Baada ya sura hii, kila mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa:
Kutumia ifaavyo ngeli za majina.
Katika kiswahili kuna ngeli nane za majina: ngeli:
a-wa,
u-i-,
ki-vi-,
li- ya-,
u-,
u-i-zi-,
pa-m-ku-
na ngeli ya **ku-**.

3.3.1 NGELI YA A- WA-

MATUMIZI YA NGELI YA a-wa-

Umoja		Wingi	
Mtu	analima	Watu	wanalima
Mzee	anakuja	Wazee	wanakuja
Ndege	anaruka	Ndege	wanaruka
Malaika	anasema	Malaika	wanasema
Kibogayo	analima	Vibogoyo	wanalima
Kiziwi	analima	Viziwi	wanalima
Mbuzi	anakula	Mbuzi	wanakula
Ng'ombe	anakula	Ngombe	wanakula

Ngeli ya -a-wa hujumuisha majina yote ya vitu vyenye uhai isipokuwa mimea kama vile watu, wanyama, ndege na Mungu, Mashetani, Malaika, Miungu n.k

VIVUMISHI VYA NGELI YA a- wa-

1. Vivumishi vya kuonyesha

Umoja	Uwingi
Mwalimu huyu anaandika	Walimu hawa wanaandika
Mwalimu huyo anaandika	Walimu hao wanaandika
Mwalimu yule anaandika	Walimu wale wanaandika

2.Vivumishi vya kumiliki(sha)

Umoja	Uwingi
Punda wako amepotea	Punda wenu wamepotea
Mzee wako anakusalimu	Wzee wenu wanawasalimu
Shetani wako amekupatosha	Mashetani wenu wamewapatosha
Punda wangu amepotea	Punda wetu wamepotea
Mzee wangu anakusalimu	Wzee wetu wanatusalimu
Shetani wangu amekupatosha	Mashetani wetu wametupatosha
Punda wake amepotea	Punda wao wamepotea
Mzee wake anakusalimu	Wzee wao wanawasalimu

Shetani wake amempotosha Mashetani wao wamewapatosha.

Tanbihi: Katika vivumishi vya kumilikisha kuna majina ya ngeli ya -a-wa- ambayo hayafuati kanuni hiyo. Mengi mwa majina hayo ni yale yanayoonyesha uhusiano wa familia.

Mfano:

1. Hatusemi baba wangu au mama wangu tunasema baba yangu, baba yako baba yake, baba yetu, baba zetu, baba zenu, shangazi yangu,..

2.Kuna pia majina ya watu yasiyofuata kanuni ya ngeli hii kama jina jambazi (hilo, hili,..)

3) Vivumishi vya kurejesha

Umoja	Uwingi
Mimi mwenyewe nililima shamba	Sisi wenyewe tulilima shamba
Mtoto mwenyewe alikimbia	Watoto wenyewe walikimbia
Mwizi mwenyewe ni huyu	Wezi wenyewe ni hawa

4. Vivumishi vya kuuliza

Umoja	Uwingi
Mwanajeshi yupi amekufa?	Wanajeshi wapi wamekufa?
Msichana yupi ameolewa?	Wasichana wapi wameolewa?
Mwanafunzi yupi amechelewa?	Wanafunzi wapi wamechelewa ?
Kibogoyo yupi amepigwa?	Kibogoyo wapi wamepigwa?
Mbuzi yupi amekinjwa?	Mbuzi wapi wamekinjwa?

5)Vivumishi vya idadi

Umoja	Uwingi
Mwalimu mmoja	Walimu wawili
	walimu watatu
	Walimu wanne
	Walimu watano
	Walimu -sita
	Walimu -saba

Walimu wanane

Walimu - tisa

Walimu - kumi

Tanbihi: Nambari sita, saba, tisa na kumi hazibadiliki katika uwingi; katika ngeli hii hazichukui kiambishi -wa-.

6) Vivumishi vya sifa

Umoja	Uwingi
Ng'ombe mkubwa	Ng'ombe wakubwa
Mpishi mpole	Wapishi wapole
Daktari mzuri	Madaktari wazuri
Msichana mrembo	Wasichana warembo.

3.3.2 NGELI YA U-I-

Baadhi ya majina ya ngeli hii ni majina ya miti, maumbile, viungo vya mwili, vifaa na matendo. Ngeli hii huchukua majina yote ambayo kwenye kitenzi huwa na kiambishi u- katika umoja, na i- katika wingi.

Yafuatayo ni baadhi yamajina ya ngeli hii: mti-miti, mkono-mikono, mchungwa-michungwa, mwili-miili, mswaki-miswaki, mlango-milango, msitu-misitu, mto-mito, msumari-misumari, mpera-mipera, mgongo-migongo, mgomba-migomba, mguu-miguu, mdomo-midomo, mlima-milima, mkondo-mikondo, mnazi-minazi, mkaba-mikaba, mkufi-mikufi,...

Tanbihi: - Katika ngeli hii kuna majina ya umoja tu kama: - Mpunga, muda (mpunga umelimwa, muda umekwisha) - Kuna vile vile majina yenye wingi tu, kama: miwani, mirathi,..

MATUMIZI YA NGELI YA u-i-

Umoja	Uwingi
Mti umeanguka	Miti imeanguka
Mkono umevunjika	Mikono imevunjika
Mchungwa una faida	Michungwa ina faida
Mwili umechoka	Miili imechoka
Mlango umefungwa	Milango imefungwa
Mto umejaa maji	Mito imejaa maji
Msumari unapigiliwa	Misumari inapigiliwa
Mpera umejaa matunda	Mipera imejaa matunda

Mnazi umekatwa	Minazi imekatwa

. VIVUMISHI VYA NGELI u-i-

a)Vivumishi vya kuonyesha

Umoja	wingi
Mlango huu umeharibika	Milango hii imeharibika
Mlango huo umeharibika	Milango hiyo imeharibika
Mlango ule umeharibika	Milango ile imeharibika

b) Vivumishi vya kumuliki

Mgomba wangu ulipandwa	Migomba yetu ilipandwa
Mgomba wako ulipandwa	Migomba yenu ilipandwa
Mgomba wake ulipandwa	Migomba yao ilipandwa

c) Vivumishivya kurejesha

Msitu wenyewe unaungua	Misitu yenyewe inaungua
Mlango wenyewe uliharibika	Milango yenyewe iliharibika
Mto wenyewe ni mkubwa	Mito yenyewe ni mikubwa

e) Vivumishi vya idadi

Umoja	wingi
Msumari mmoja	Misumari miwili
	Misumari mitano
	Misumari -sita
	Misumari -saba
	Misumari minane
	Misumari -tisa
	Misumari -kumi
	Misumari mia moja
	Misumari mingi

f)Vivumishi vya kuuliza

Umoja	Uwingi
Mti upi umekatwa?	Miti ipi imekatwa?
Mchungwa upi umezaa matunda?	Michungwa ipi imezaa matunda?
Mguu upi umevunjika?	Miguu ipi imevunjika?

g) Vivumishi vya sifa

Mti mkavu	Miti mikavu
Mti mzuri	Miti mizuri
Mti mfupi	Miti mifupi

3.3.3 NGELI YA KI-VI

Ngeli hii huchukua majina ya vitu pamoja na viungo vya mwili; imeitwa ngeli ya ki-vi-kwa sababu hutambulishwa na kiambishi **ki**- katika umoja na **vi**- katika wingi. Yafuatayo ni baadhi ya majina ya ngeli hii: Kisu-visu, kijiko-vijiko, kikapu-vikapu, kiuno-viuno, kichwa-vichwa, kisiginovisigino, kikombe-vikombe, kiti-viti, kiwiko-viwiko, kioo-vioo, chuma-vyuma, chumba-vyumba, chombo-vyombo, choo-vyoo,...

MATUMIZI YA NGELI YA ki -vi-

Umoja	wingi
Kikombe kimevunjika	Vikombe vimevunjika
Kisu kimepotea	Visu vimepotea
Kitabu kimechafuka	Vitabu vimechafuka
Kijiko kimeanguka	Vijiko vimeanguka
Choo kimejaa	Vioo vimejaa
Kiberiti kinawaka	Viberiti vinawaka
Chumba kilifunguliwa	Vyumba vilifunguliwa
Kiti kimekaliwa	Viti vimekaliwa
Kitambaa kitafuliwa	Vitambaa vitafuliwa
Chungu kinasafishwa	Vyungu vinasafishwa

VIVUMISHI VYA NGELI ki-vi

a) Vivumishi vya kuonyesha

Umoja	wingi

Kitabu hiki kinapendeza — Vitabu hivi vinapendeza

Kitabu hicho kinapendeza — Vitabu hivyo vinapendeza

Kitabu kile kinapendeza — Vitabu vile vinapendeza

b) Vivumishi vya kumiliki

Umoja — wingi

Kiti changu kimevunjika — Viti vyetu vimevunjika

Choo chako kimejaa — Vyoo vyenu kimejaa

Kiberiti chake kimekwisha — viberiti vyao vimekwisha

c) Vivumishi vya kurejesha

Kioo chenyewe kimepasuka — Vioo vyenyewe vimepasuka

Chungu chenyewe kimetoboka — Vyungu vyenyewe vimetoboka

Kisu chenyewe kimenolewa — Visu vyenyewe vimenolewa

d) Vivumishi vya kuuliza

Kiberiti kipi kimewaka? — Viberiti vipi vimewaka?

Kiberiti gani kimewaka? — Viberiti gani vimewaka?

Kisu kipi ni kizuri? — Visu vipi ni vizuri?

e) Vivumishi vya idadi

Umoja — wingi

Kitabu kimoja kimeibwa — Vitabu viwili vimeibwa

Vitabu vitatu vimeibwa

Vitabu vine vimeibwa

Vitabu vitano vimeibwa

Vitabu –sita vimeibwa

f) Vivumishi vya sifa

Kitabu kizuri — Vitabu vizuri

Kitambaa kirefu — Vitambaa virefu

Kisu kipya — Visu vipya

3.3.4 NGELI YA LI-YA-

Majina yanayoingia katika ngeli hii huwa na umoja na wingi. Wingi wa majina ya ngeli hii hupatikana kwa kupachikwa viambishi *ma-*. Yafuatayo ni baadhi ya majina ya ngeli hii: jibu-majibu, jani-majani, jeshi-majeshi, jeneza-majeneza, jambazi-majambazi, jengomajengo, jukwaa-majukwaa, jini-majini, jaribio-majaribio, jeraha-majeraha, kabati-makabati, jiwe,mawe, bega-mabega, gurudumu-magurudumu, gari-magari, dirisha-madirisha, koti-makoti, shamba-mashamba, shati-mashati, chungwa-machungwa, pera-mapera,....

TANBIHI : Maneno machacke katika ngeli hii uwingi wake hupatikana kwa kupachika kiambishi ma- tu, bali kwa kuondoa silabi ya kwanza na kupachika ma au me.

Mfano : Jicho = macho

Jambo = mambo Jiwe = mawe Jino = meno

MATUMIZI YA NGELI YA li-ya-

Umoja	wingi
Jahazi limezama baharini	Majahazi yamezama baharini
Jibu limepatikana	Majibu yamepatikana
Jino limeng'oka	Meno yameng'oka
Gari limekwama mchangani	Magari yamekwama mchangani
Jambazi litakamatwa jana	Majambazi yamekamatwa
jana Jipu litapasuliwa hospitalini	Majipu yatapasuliwa hospitalini
Jicho linaniuma	Macho yananiuma
Kabati limeingizwa chumbani	Makabati yameingizwa chumbani

VIVUMISHI VYA NGELI YA li-ya-

a)***Vivumishi vya kuonyesha***

Umoja	wingi
Ganda hili linateleza	Maganda haya yanateleza
Ganda hilo linateleza	Maganda hayo yanateleza
Ganda lile linateleza	Maganda yale yanateleza

b)Vivumishi vya kumiliki

Umoja	wingi

Koti langu limeibwa	Makoti yetu yameibwa
Koti lako limeibwa	Makoti yenu yameibwa
Koti lake limeibwa	Makoti yao yameibwa

c)Vivumishi vya kurejesha

Umoja	wingi
Jipu lenyewe limeiva	Majipu yenyewe yameiva
Shamba lenyewe linalimwa	Mashamba yenyewe yamelimwa

d)Vivumishi vya kuuliza

Umoja	wingi
Jukwaa lipi tutaonyeshea?	Majukwaa yapi tutaonyeshea?
Jiwe lipi amekutupia?	Majiwe yapi amekutupia?
Juma gani tutapumuzika?	Majuma gani tutapumuzika?

e)Vivumishi vya idadi

Umoja	wingi
Shamba moja limelimwa	Mashamba mawili yamelimwa
	Mashamba matatu yamelimwa
	Mashamba manne yamelimwa
	Mashamba matano yamelimwa
	Mashamba -sita yamelimwa
	Mashamba -saba yamelimwa
	Mashamba manne yamelimwa
	Mashamba manne yamelimwa

f) Vivumishi vya sifa

Jengo refu limeanguka	Majengo marefu
Jiwe kubwa limepasuka	Majiwe makubwa
Kabati zuri limenunuliwa	Makabati mazuri

Jeneza fupi limetengenezwa Majeneza mafupi yametengenezwa

3.3.5 NGELI YA U-

Ngeli hii huchukua majina ya dhahania, (majina ya maarifa) kiamishi ngeli katika kitenzi ni u- katika umoja na uwingi Yafuatayo ni baadhi ya majina ambayo yamo katika ngeli hii: ulafi, uzembe, ukubwa, unene, wembamba, weusi, ujinga, ujana, ulaghai, ujuzi, uzee, utajiri, umasikini, wekundu, uchovu, ubahili, ulevi, utakatifu, uovu, ivivu, ukatili...

MATUMIZI YA NGELI YA u-

Umoja	wingi
Ukubwa unampa kiburi	Ukubwa unawapa kiburi
Unene unamletea jasho	Unene unawaletea jasho
Weusi unampendeza	Weusi unawapendeza
Ujinga ulimdunisha	Ujinga uliwadunisha
Uzungu unampumbaza	Uzungu unawapumbaza
Werevu umenizidi	Werevu umewazidi
Utajiri unamzuaza	Utajiri unawazuaza
Uzembe unanichukiza	Uzembe unawachukiza
Utani unaniudhi	Utani unatuudhi

VIVUMISHI VYA NGELI YA u-

a) Viambishi vya kuonyesha

Unene huu mzuri

Unene huo mbaya

Unene ule unanitia

b) Vivumishi vya kumiliki

Weusi wangu unapendeza

Weusi wetu unapendeza

Weusi wako unapendeza

Weusi wenu unapendeza

Weusi wake unapendeza

Weusi wao unapendeza

c) Vivumishi vya kurejesha

Uzuri wenyewe umemtoka

Uzuri wenyewe umewatoka

Ujuzi wenyewe ni wa kulazimisha

d)Vivumishi vya kuuliza

Umoja	wingi
Unafiki upi unakuchukiza ?	Unafiki upi unawachukiza?
Ukarimu gani unazungumzia?	Ukarimu gani mnazungumzia?
Ujinga upi umezidi?	Ujinga upi umemzidi?

e) Vivumishi vya idadi : Ngeli hii haiendi na idadi

g) Vivumishi vya sifa

Utajiri mkubwa

Weusi mzuri

Ujuzi mdogo

3.3.6 NGELI YA U-I-ZI

Majina yaliyomo katika ngeli hii hutambulishwa na viambishi ngeli ***u***-na ***i***- katika umoja, na ***zi-*** katika uwingi. Yafuatayo ni baadhi ya majina ya ngeli hii: ubao-mbao, ufunguo-funguo ukuta-kuta, wavu-nyavu, ukucha-kucha, ufagio-fagio, ufito-fito, wayo-nyayo, wimbo-nyimbo. ulimi-ndimi, uso-nyuso,.... barabara-barabara, njia-njia, alama-alama, sauti-sauti, nyumba-nyumba, suruali-suruali, akili-Akili, baiskeli-baiskeli, kalamu-kalamu, karatasi-karatasi, ndege-ndege,....

MATUMIZI YA NGELI HII

Umoja	wingi
Barabara imenyooka	Barabara zimenyooka
Sauti imesikikaka	Sauti zimesikika
Baiskeli imeibwa	Baiskeli zimeibwa
Kalamu inaandika	Kalamu zinaandika
Ukuta umebomoka	Kuta zimebomoka
Wimbo unafurahisha	Nyimbo zinafurahisha

Ufunguo umepotea	Funguo zimepotea
Unyasi umekauka	Nyasi zimekauka

VIVUMISHI VYA NGELI YA u-i-zi-

a) Vivumishi vya kuonyesha

Karatasi hii imechanika	Karatasi hizi zimechanika
Karatasi hiyo imechanika	Karatasi hizo zimechanika
Karatasi ile imechanika	Karatasi zile zimechanika
Wavu huu umekatika	nyavu hizi zimekatika
Wavu huo umekatika	nyavu hizo zimekatika
Wavu ule umekatika	nyavu zile zimekatika

b) ***Vivumishi vya kumiliki***

Ndege yangu imeanguka	Ndege zetu zimeanguka
Ndege yako imeanguka	Ndege zakozimeanguka
Ulimi wangu umeumia	Ndimi zetu zimeumia
Ulimi wako umeumia	Ndimi zenu zimeumia
Ulimi wake umeumia	Ndimi zao zimeumia

c) ***Vivumishi vya kurejesha***

Umoja	wingi
Akili yenyewe imevurugika	Akili zenyewe zimevurugika
Suruali yenyewe imechafuka	Suruali zenyewe zimechafuka
Baiskeli yenyewe imeibwa	Baiskeli zenyewe zimeibwa
Uzi wenyewe umekatika	Nyuzi zenyewe zimekatika
Ubao wenyewe umefutwa	Mbao zenyewe zimefutwa
Ufunguo wenyewe umepotea	Funguo zenyewe zimepotea

d) Vivumishi vya kuuliza

Umoja	wingi
Suruali ipi inakubana?	Suruali zipi zinawabana?
Karatasi ipi/gani imechanika?	Karatasi zipi/gani zimechanika?
Ndege ipi imeanguka?	Ndege zipi zimeanguka?
Wimbo upi umekufurahisha?	Nyimbo zipi zimekufurahisha?
Uso upi unakupendeza?	Nyuso zipi zinakupendeza?
Ukucha upi/gani umerefuka?	Kucha zipi/gani zimerefuka?

e) Vivumishi vya idadi

a) Ndege -moja imepotea	Ndege mbili zimepotea

Ndege -tatu zimepotea

Ndege -nne zimepotea

Ndege -tano zimepotea

Ndege -sita zimepotea

Ndege -saba zimepotea

Ndege -nane zimepotea

Ndege -tisa zimepotea

Ndege -kumi zimepotea

Ndege ishirini zimepotea

b) Wembe mmoja umeibwa

Nyembe mbili zimeibwa

Nyembe -tatu zimeibwa

Nyembe- nne zimeibwa

Nyembe -tano zimeibwa

Nyembe- sita zimeibwa

Nyembe -saba zimeibwa

Nyembe -nane zimeibwa

Nyembe -tisa zimeibwa

Nyembe -kumi zimeibwa

Nyembe- ishirini zimeibwa

f)Vivumishi vya sifa

Nyumba nzuri imejengwa	Nyumba nzuri zimejengwa
Kalamu ndefu inaandika	Kalamu ndefu zinaandika
Baiskeli mpya inauzwa	Baiskeli mpya zinauzwa
Karata nyepesi imechanika	Karata nyepesi zimechanika
Ufa mkubwa umezibwa	Nyufa kubwa zimezibwa
Ufagio mrefu umepotea	Fagio ndefu zimepotea
Ubao mweusi umefutwa	Mbao nyeusi zimefutwa

3.3.7 NGELI YA PA-M-KU-

Ngeli hii huchukua majina yote ya mahali. Viambishi ngeli vyake ni ***pa-m-ku-*** katika vitenzi. Kwa kawaida katika ngeli hii mahali panapozungumziwa panaweza kujulikana kwa ujumla (pa-), kwa wazi wazi (ku-) au pakawa ndani ya kitu (m-).

MATUMIZI YA NGELI HII

Umoja	Uwingi
Butare pamechafuka	Butare pamechafuka
Ofisini mna nyoka	Maofisini mna nyoka
Hospitalini kuna maajabu	Mahospitalini kuna maajabu
Ziwani mna samaki	Maziwani mna samaki
Sokoni kuna chakula	Masokoni kuna chakula
Ruhengeri kuna mlima	Ruhengeri kuna milima
Kichwani pananiwasha	Vichwani pananiwasha
Mguuni pamevimba	Miguuni pamevimba
Kitabuni mna hadithi tano	Vitabuni mna hadithi tano
Msituni kuna wanyama	Misituni kuna wanyama

VIVUMISHI VYA NGELI YA pa-m-ku-

a) Vivumishi vya kuonyesha

-pa-

Mahali hapa pana maji

Mahali hapo pana maji

Mahali pale pana maji

-m-

Chumbani humu mna joto

Chumbani humo mna joto

Chumbani mle mna joto

-ku-

Msituni huku kuna simba

Msituni huko kuna simba

Msituni kule kuna simba

b)Vivumishi vya kumiliki

-pa-

Umoja	Uwingi
Mahali pangu pamefagiliwa	Mahali petu pamefagiliwa
Mahali pako pamefagiliwa	Mahali penu pamefagiliwa
Mahali pake pamefagiliwa	Mahali pao pamefagiliwa

-m-

Umoja	Uwingi
Chumbani mwangu mmechafuka	Chumbani mwetu mmechafuka
Chumbani mwako mmechafuka	Chumbani mwenu mmechafuka
Chumbani mwake mmechafuka	Chumbani mwao mmechafuka

c)Vivumishi vya kurejesha

-pa-

Mahali penyewe panaogopesha

Uwanjani penyewe panateleza

-m-

Ndani mwenyewe mnanuka vizuri

Mtoni mwenyewe mna mamba

-ku-

Nje kwenyewe kuna joto

Shambani kwenyewe kuna simba

d)Vivumishi vya kuuliza

Mahali papi panapendeza?

Mahali kupi kunapendeza?

Mahali mpi mnapendeza?

e)Vivumishi vya idadi

Mahali pamoja

Mahali pawili

Mahali patatu

Mahali panne

Mahali patano

Mahali sita

Mahali saba

Mahali kumi

Mahali vya pengi

f)Vivumishi sifa

Mahali pachafu patafagiliwa

Mahali kuchafu kutafagiliwa

Mahali mchafu mtafagiliwa

Sokoni pasafi patauzwa chakula

MAZOEZI

a) Changua neno lililo sahihi na kuliandika katika nafasi wazi

1) Humu ndimo chumbani ..... joto (palimo, mlimo, mlipo,uliko)

2) Mahali ..... rutuba panastawi mimea (mliko, paliko, palipo, ziliwo)

3) Ndani ya bahari hii ..... samaki wakubwa sana (pana, mna, ipo, zipo)

4) Chumbani ..... mna giza sana (wangu, pangu, mwangu

5) Shureni kwetu ni ..... mno (kuzuri, vizuri, mzuri, zuri)

6) Mvua ilinyesha mahali ..... (kwingi, wengi, nyingi, pengi)

7) Kazini ..... ni mbali na hapa?(yupi, kupi, kipi, ipi)

8) Huyu ndiye mwalimu ..... tulikuwa tukimsema (mwenyewe, wenyewe, kwenyewe)

3.3. 8 NGELI YA KU-

Ngeli hii inaainisha vitenzijina, yaani majina yanayo umbo la kitenzi kama, kuimba, kucheza, kucheka , kulima, kujifunza,...

MATUMIZI YA NGELI HII.

Umoja	Uwingi
Kucheza kumemchokesha	Kulima kuliwatajirisha
Kuimba kunamfurahisha	Kukimbia kumewaokoa
Kusali kutamfariji	Kukoroma kuliwatisha
Kulewa kumemponza	Kuumwa kumewakondesha
Kucheka kunampendeza	Kucheza kumewachokesha
Kulima kulimtajirisha	Kuimba kunawafurahisha
Kukimbia kumemuokoa	Kusali kutawafariji
Kukoroma kulimtisha	Kulewa kumewaponza
Kuumwa kumemkondesha	Kucheka kunawapendeza

VIVUMISHI VYA NGELI HII

a) **VIVUMISHI VYA KUONYESHA**

Kuimba huku kubaya.

Kulima huko kutawachokesha

Kunywa kule kunalevya

b) **VIVUMISHI VYA KUMILIKI**

Kukimbia kwangu kumepungua.
Kuimba kwako kumetufurahisha.
Kunywa kwake kumemuua.

Kukimbia kwetu kumepungua.

Kuimba kwenu kumetufurahisha.

Kunywa kwao kumemuua.

c) **VIVUMISHI VYA KUREJESHA**

Kusali kwenyewe kumekwisha.
Kusoma kwenyewe kubaya.
kunywa kwenyewe kumezidi.

d) **VIVUMISHI VYA KUULIZA**

Kuvaa kupi kunapendeza?
Kuandikwa kupi kunatakiwa?
Kuimba gani kutashinda?

e) **VIVUMISHI VYA SIFA**

Kuimba kuzuri kumesifiwa.

Kucheza kubaya kumekwisha.

Kutembea kurefu kumetuchokesha.

3.3.9 MAJINA KUBADILI NGELI

Kuna wakati ambapo majina huweza kubadili ngeli na kuwa katika ngeli nyingine. Hali hiyo hujitokeza mara nyingi katika kudunisha na kukuza majina, ili kupunguza au kuongeza maana yake ya kawaida.

HALI YA KUDUNISHA MAJINA

Kudunisha majina ni kuyapa maana inayopunguza ukubwa au unene wake. Katika hali hii tunaweka majina ya ngeli nyingine katika ngeli ya ki-vi-

Mfano :

Hali ya kawaida	Hali ya kudunisha
Ulima-milima(u-i) {umusozi/imisozi}	kilima- vilima (ki-vi) {agasozi/udusozi}
Sanduku-masanduku (li-ya)	kisanduku-visanduku
Mtoto –watoto (a-wa-)	kitoto-vitoto
Tonge-matonge (li-ya-)	kitonge-vitonge
Tumbo-matumbo (li-ya-)	kitumbo-vitumbo
Vumbi-mavumbi (li-ya-)	kivumbi-vivumbi
Nyumba-nyumba (i-zi-)	kinyumba-vinyumba

TANBIHI:

1.Katika kudunisha, wakati ambapo shina la neno ni silabi moja tu, tunapaswa kupachika -ji-katikati.

Mifano:

Hali ya kawaida	Hali ya kudunisha
Mti-miti	kijiti-vijiti
Mwiko-miiko	kijiko-vijiko
Mto-mito	kijito-vijito
Mtu-watu	kijitu-vijitu

2.Wakati nomino huanzia na ki- tunapaswa vile vile kupachika ji katikati.

Mifano:

Hali ya kawaida	Hali ya kudunisha
Kiboko-viboko	kijiboko-vijiboko
Kichwa-vichwa	kijichwa-vijichwa
Kitabu-vitabu	kijitabu-vijitabu
Kiatu-viatu	kijiatu-vijiatu

. HALI YA KUKUZA MAJINA

Katika hali ya kukuza ni kugeuza maana ya kawaida ya majina na kuyapa maana ya kuonyesha ukubwa. Kukuza majina ni kuweka majina ya ngeli nyingine katika ngeli ya li-ya-.

Mfano:

Hali ya kawaida	Hali ya kukuza
Mtu(a-wa-)	Jitu-majitu(li-ya-)
Nyumba(u-i-zi-)	Jumba-majumba(li-ya-)
Mfuko-mifuko(u-i-)	Jifuko-majifuko (Li-ya-)
Mwizi-wezi (a-wa-)	Jizi-majizi (li-ya)
Mbwa (a-wa-)	Jibwa -majibwa(li- ya-)
Kisu (ki-vi-)	visu (ki-vi-)
Mke (a-wa-)	Jike-majike (a-wa-)
Mti-miti(u-i-)	Jiti- majiti (li- ya-)

JADWALI YA NGELI ZA KISWAHILI

Ngeli ya:	Mwanzo wa jina	Kiambishi nafsi yakinishi	Kiambishi nafsi kanushi	Mfano	Mf. wa Kivumishi cha kuonyesha		
					karib	Karibu	Mbali

					u	nawe	nami
a- wa-	m / mw- wa-	ni- u- a- tu- m- wa-	si- hu- ha- hatu- ham- hawa-	mtu watu	huyu hawa	huyo hao	yule wale
u- i-	m / mw- mi-	u- i-	hau- hai-	mlima milima	huu hii	huo hiyo	ule ile
Ki- vi-	Ki/ch- vi/vy-	Ki- vi-	haki- havi-	kisu visu	hiki hivi	Hicho hivyo	Kile vile
li- ya-	(ji-)… ma-	li- ya-	hali- haya-	Jembe majembe	hili haya	hilo hayo	Lile yale
U-	u-	u-	Hau-	uzuri	huu	huo	ule
u- i- zi-	u- n- n-	u- i- zi-	hau- hai- hazi-	uso nyumba nyuso	huu hii hizi	huo hiyo hizo	Ule Ile zile
Pa- Mu- Ku-	hutegemea na mahali	pa- mu- ku-	hapa- ham- haku-	mahali chumbani sokoni	hapa humu huku	hapo humo huko	Pale Mle kule
Ku-	ku-	ku-	haku-	kucheza	huku	huko	kule

SEHEMU YA NNE: KUKUZA MSAMIATI

SHABAHA ZA SOMO HILI

Baada ya sura hii, kila mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa:
1.Kutumia msamiati kuhusu hesabu tofauti
2.Kuandika hesabu tofauti.
3.Kutumia istalahi ifaavyo kulingana na mazingira

4.1 HESABU /TARAKIMU

0: Sufuri

1: moja

2 : mbili

3: tatu

4: nne

5: tano

6: sita

7: saba

8 :nane

9: tisa

10: kumi

11: kumi na moja

12: kumi na mbili

13: kumi na tatu

14: kumi na nne

15: kumi na tano

16: kumi na sita

17: kumi na saba

18: kumi na nane

19: kumi na tisa

20: ishirini

21: ishirini na moja

22: ishirini na mbili

10: kumi

20: ishirini

30: thelathini

40: arobaini

50: hamsini

60: sitini

70: sabini

80: themanini

90: tisini

100: mia moja

101: mia moja na moja

102: mia moja na mbili

200: mia mbili

300: mia tatu

400: mia nne

500: mia tano

600: mia sita

700: mia saba

800: mia nane

900: mia tisa

1000: elfu moja

1,001: elfu moja na moja

1,002: elfu moja na mbili

1,010: elfu moja na kumi

1,011: elfu moja na kumi na moja

1,028: elfu moja ishirini na nane

1,100: elfu moja na mia moja

1,101: elfu moja na miamoja na moja

1,999: elfu moja, mia tisa tisini na tisa

2,000: elfu mbili

3,000: elfu tatu

4,000: elfu nne

5,000: elfu tano

6,000 :elfu sita

7,000: elfu saba

8,000 :elfu nane

9,000: elfu tisa

10,000: elfu kumi

100,000: elfu mia moja au **laki moja**

200,000: elfu mia mbili au laki mbili

1,000,000: milioni moja

1**,000,000,000**: bilioni moja

1,234,567,890: Bilioni moja, milioni mbili thelathini na nne, laki tano sitini na saba,

mia nane na tisini.

592,325 : laki tano, tisini na mbili, mia tatu ishirini na tano.

ZOEZI:

i) Andika kwa maneno:

574,205

1,572,320

1,572,328

3,698,500

1,572,300

9,999,999

a) KUANDIKA DESIMALI

1.1: moja nukta moja

1.2: moja nukta mbili

1.25: moja nukta mbili tano

5.105: tano nukta moja moja sufuri tano

10.1: kumi nukta moja

100.15: mia moja nukta moja tano

b) SEHEMU

½: nusu

1/3: thelusi moja

2/3: theluthi mbili

¼: robo

1/6 sudusi

1/5: moja kwa tano (Humusi)

1/7: moja kwa saba (SUBUI)

1/100: moja kwa mia (USHURU)

1/8:thumuni

1/9: tusui

2/10: mbili kwa kumi

25/750: ishirini na tano kwa mia saba na hamsini

c) ASILIMIA

20%: asilimia ishirini

50%: asilimia hamsini

25%: asilimiaishirini na tano

78%: asilimia sabini na nane

4.2 SIKU ZA WIKI(JUMA)

Jumamosi

Jumapili

Jumatatu

Jumanne

Jumatano

Alhamisi

Ijumaa

Jumamosi

Jumapili

4.3 MIEZI YA MWAKA

Mwezi una majuma manne

Juma moja ina siku saba

Mwaka una miezi kumi na miwili

Haya yafuatayo ni majina ya miezi katika Kiswahili:

Mwezi wa kwanza = Januar

i Mwezi wa pili = Februari

Mwezi wa tatu = Machi

Mwezi wa nne = Aprili

Mwezi wa tano = Mei

Mwezi wa sita = Juni

Mwezi wa saba = Julai

Mwezi wa nane = Agosti

Mwezi wa tisa = Septemba

Mwezi wa kumi = Octoba

Mwezi wa kumi na moja = Novemba

Mwezi wa kumi na mbili = Disemba

4.4 SAA

9:00: saa tatu kamili

9:05 : saa tatu na dakika tano

9:15 ; saa tatu na robo

9:25 :saa tatu na dakika ishirini na tano

9:30 : saa tatu na nusu

9:40 : saa tatu na dakika arobaini

9:45 : saa nne kasorobo

9:50 : saa nne kasoro dakika kumi

8:00 : saa mbili kamili

7:00 : saa moja kamili

6:00 : saakumi na mbili kamili

10:00 : saa nne kamili

11:00: saa tano kamili

12:00: saa sita kamili

13:00 ; saa saba kamili

14:00 :saa nane kamili

15:00 : saa tisa kamili

16:00 : saa kumi kamil

17:00 : saa kumi na moja kamili

18:00: saa kumi na mbili kamili

22;15: saa nne na robo za usiku

23:45: saa sita kasorobo za usiku

4.5 ALAMA ZA HESABU

+ (Alama ya kujumlisha)

- (alama ya kutoa au kuondoa)

X (alama ya kuzidisha)

÷ Alama ya kugawanya (kugawa)

= Alama ya kusawazisha (alama ya sawa sawa)

% (Alama ya asilimia)

< (Alama ya ndogo kuliko)

> (Alama ya kubwa kuliko)

( ) (Alama ya mabano au kifungio) au mabano ya mduara

[ ] Mabano ya mraba

/ Alama ya mkwaju

4.6 MAUMBO

Kuna maumbo mbali mbali yanayojulikana. Baadhi ya maumbo hayo tunaweza kusema:

1. Mraba (square): Mraba ni umbo la pande nne ambalo upana na urefu ni sawa na hufanya pembe za digri tisini.

2. Mstatili (Rectangle): Ni umbo lenye pembe nne na pande nne, kila mbili zinazokabiliana zinalingana vipimo na kila pembe yake huwa na digri tisini.

3. Pembe tatu (triangle): Ni umbo liloundwa kwa mistari mitatu inayokutana katika ncha tatu. Pembe tatu huwa na aina mbali mbali; kwa mfano:

Pembe tatu mraba: Ni umbo lenye mistari mitatu ambalo mistari yake miwili hukutana katika ncha yenye digri tisini.

Pembe tatu pacha: Ni umbo liloundwa kwa mistari mitatu inayokutana katika ncha mbili zinazolingana yaani kuna pande mbili sawa.

Pembe tatu sawa: Ni umbo linaloundwa kwa mistari mitatu inayokutana katika ncha tatu zinazolingana, yaani pande zake zote ni sawa.

1. **Duara (cercle):** Ni umbo la mvilingo, mzunguko au umbo la yai (duara dufu)
2. **Duaradufu : N**i umbo la yai.
3. **Nusu duara :** ni kipande kimoja cha duara iliyopasuliwa katika vipande viwili sawa.
4. **Kipenyo :** ni mstari ulionyoka unaopita katikati ya duara.
5. **Nusukipenyo :** ni mstari utokao katikati ya duara mpaka kwenye kizingo chake.

6. **Mchemraba :** ni kitu chenye umbo lenye nyuso sita za mraba.
7. **Mchemstatili :** Ni kitu chenye umbo lenye nyuso sita za mstatili.

4.7 RANGI MBALIMBALI

Katika mazingira yetu tunakutana na rangi tofauti. Ingawa rangi zipatikanazo ni nyingi sana, tutajaribu kupitia chache miongoni mwake. Rangi hizo ni kama hizi zifuatazo :

1.Rangi nyeupe : Ni rangi yenye mwangaza, isiyo na giza, iliyo safi.

2.Rangi nyeusi : Ni rangi yenye giza, yenye utusitusi, isiyo na uzuri, kinyume cha nyeupe.

3.Rangi nyekundu : Ni rangi ifananayo(inayofanana) na damu.

4.Rangi ya manjano(njano) : Ni rangi kama ya ganda la ndimu au limau lililoiva.

5.Rangi ya kijani : Ni rangi inayofanana na majani.

6.Samawati au buluu : Ni rangi ya mbingu inayoonekana wakati hakuna mawingu.

7.Zambarau : Urujuani

8.Chungwa : Ni rangi inayofanana na tunda linaloitwa chungwa.

9.Hudhurungi : Ni rangi inayofanana na maji ya kahawia.

10.Waridi : Ni rangi ya mojawapo ya ua linalonukia vizuri.

11.Jivujivu(kijivu) : Ni rangi linalofanana na jivu.

4.8 UHUSIANO WA FAMILIA

Tunapozungumzia uhusiano wa familia kuna elementi muhimu za kufuatilia au za kuzingatia:

-Baba, Mama, wazazi, Mume,Mke.

-Mvulana (mtoto wa kiume), msichana (mtoto wa kike).

-Kaka, dada, ndugu, watoto.

-Babu, nyanya(bibi), wajukuu(mjukuu).

-Mjomba, wapwa(mpwa), shangazi.

-Baba mdogo, kaka kwa baba mdogo, dada kwa baba mdogo, baba mkwe.

-Mama mkwe, shemeji, mama mdogo.

Uhusiano wa familia unatokana na pande mbili muhimu. Pande hizo ni kama zifuatazo :

-Uhusano wa mume, mke, watoto na ndugu kwa upande wa mume.

-Uhusiano wa mume, mke, watoto na ndugu kwa upande wa mke.

Muhimu :

1. **Babu :** Ni Baba mzaa wa Baba au mama.
2. **Nyanya (Bibi) :** Ni mama mzaa wa baba au mama.
3. **Shangazi :** Ni dada ya baba wa mtu au ndugu wa kike wa baba.
4. **Mjomba :** Ni kaka ya mama wa mtu au ndugu wa kiume wa mama (kaka wa mama).
5. **Wapwa :** Ni watoto wa dada ya mtu ambaye ni mwanamume.
6. **Ndugu:** Ni watoto wanaozaliwa tumbo moja. Yaani ni ndugu kwa wazazi wote wawili.
7. **Wazazi:** Ni baba na mama wa mtu au watu.
8. **Mvulana :** Ni mtoto wa kiume.
9. **Msichana :** Ni mtoto wa kike (Binti).
10. **Binti:** Ni mtoto wa kike ambaye hajaolewa au hajafunga ndoa.
11. **Mwanaume:** Ni mtoto wa kiume (Mvulana) amabaye ameisha funga ndoa.
12. **Mwanamke:** Ni mtoto wa kike au msichana ambaye ameisha funga ndoa, au mtoto wa jinsia ya kike.
13. **Mkwe(mcheja):** Mzazi wa mke au mume wa mtu.
14. **Baba mkwe:** Ni Baba wa mke au mume wa mtu.
15. **Mama mkwe:** Ni mama wa mke au mume wa mtu.
16. **Baba wa kambo :** Mwanamume asiyekuwa baba yako, lakini ni mume wa mama yako au anakulea tu. Yaani hamna uhusiano wa damu.
17. **Mama wa kambo :** Mwanamke asiyekuwa mama yako, lakini ni mke wa baba yako au anakulea tu. Yaani hamna uhusiano wa damu.
18. **Mtoto wa kambo :** Mtoto ambaye hamna uhusiano wa damu. Yaani si mtoto kutoka tumboni mwako.
19. **Shemeji :** Ni kaka na dada ya mke au mume wa mtu.
20. **Mama mdogo :** Ni ndugu wa kie wa mama ya mtu.
21. **Mjukuu :** Ni mtoto wa mtoto wa mtu.
22. **Kitukuu(mtukuu) :** Ni mtoto wa mjukuu.
23. **Kilembwe :** Ni mtoto wa kitukuu(mtukuu).
24. **Kilembwekeza(kinying'inia) :** Ni mtoto aliyezaliwa na kilembwe.
25. **Mavyaa :** Jina ambalo hutumiwa katika kuitana baina ya mke na mama wa mume wake.
26. **Pacha :** Watoto waliozaliwa kutokana na mimba moja.

4.9 SEHEMU ZA MWILI

Kwanza, mwili wa binadamu unagawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu hizo ni: **Kichwa, Kiwiliwili na miguu.**

Magofu huonyesha **fuvu** ambalo ndilo nyumba ya ubongo kichwani; **mtulinga** ambao ni mfupa uzungukao shingo kwa mbele; **mbavu** ambazo ndizo nyumba ya moyo na viungo vingine **kifuani**; **uti wa mgongo** ambao ndio njia ya **neva**(mshipa wa fahamu) na **kombe** la bega kwa nyuma. Kadhalika, **gofu** pia lina **fupa la mgongo** ambalo huunganisha **paja** na **kiuno**; **kifandugu** ambacho ndicho kifupa cha mwisho kabisa cha uti wa mgongo; **pia ya goti** ambayo ni kifupa mbele ya **goti** ambacho huchezacheza kinaposhikwa; **muundi** ambao ni mfupa wa mbele wa miguu; **mifupa ya mikono** na hata **jicho la miguu** ambacho ni kifupa upande huu na huu wa mguu wa chini. Ni sehemu hizi basi ambazo zikiwa na nyama huitwa mwili wa binadamu.

Mwili wa binadamu una sehemu chungu nzima. Sehemu hizo, ukianza kwa juu kichwani, ni kama vile **utosi, nywele, paji, komo, kogo, ushi, ukope, mashavu, uso, pua, mdomo, mwanya, kidevu,** na **sikio.** Kama ujuavyo, **utosi** ni katikati ya kichwa kwa juu. **Paji** ni sehemu ya juu ya uso. Lakini **komo** na **kogo** ni tofauti. **Komo** ni paji la uso lililotokezea, nayo kogo ni sehemu ya nyuma ya kichwa hasa iliyotokezea pia. Hata hivyo, **kisogo** ni sehemu ya nyuma ya kichwa.

Kuna pia **mdomo, pua, sikio, mashavu, kidevu, ushi(nyusi)** na **ukope(kope). Nyusi** ni nywele za jicho kwa juu, yaani ziko juu ya jicho kidogo. Lakini **kope** ni nywele ziotazo kwenye kikawa cha jicho. Pia **ukope** ni ngozi ifunikayo jicho. **Mwanya** ni nafasi iliyo katikati ya meno au uwazi uliopo baina ya meno mawili hasa ya mbele. Usoni, pana **jicho**. Sehemu katikati ya jicho huitwa kiini cha jicho ama mboni ya jicho.

Hali kadhalika, zipo **ndevu** usoni. Jina ndevu ni jina la jumla lakini mtu anaweza akanyoa na kuacha mstari wa ndevu kutoka sikio hadi hili hadi jingine. Hizi huitwa **sharafa.** Pengine, mtu anaweza kunyoa na kuacha ndevu chini ya mdomo wa chini. Hizi nazo huitwa **kionjamchuzi** au **kirambamchuzi**. Unaweza pia kunyoa na kuacha tu ndevu za juu ya mdomo. Hizi huitwa **masharubu.** Nazo ndevu ziachwazo kwenye kidevu pekee, huitwa **kidevu** hivyo hivyo.

Ukitoka kichwani, unapata sehemu kama vile **shingo, kifua, kwapa, mikono, kiganja(viganja) au kitanga, kifundo cha mkono, kiwiko(**kiungo kinachounganisha kiganja na sehemu ya juu ya mkono**), kitengele(**sehemu ya katikati mwa kiganja), **kilimbilimbi, kucha, kisugudi(kiko), vidole, bega, matiti(chuchu), mgongo, tumbo, kitovu, kinena(**kinena ni sehemu ya mwili iliyo baina ya tumbo na tupu**).** Sehemu hii ya kinena ndiyo inayootea manyoya ajulikanayo kwa jina la **mavuzi.** Chini ya kinena kidogo kuna viungo vya kijinsia, yaani uume na uke ambavyo ni **mboo** na **mapumbu** kwa mwanamume; na **kuma** kwa mwanamke**. Makalio(matako), kiuno, paja, goti(magoti), pia ya goti** au **kilegesambwa , mguu(miguu), jicho la mguu(nguyu) au kifundo cha mguu, kisigino, wayo(sehemu ya chini ya mguu inayokanyaga)** na **vidole vya miguu.**

Kitanga cha mkono kinakuwa na vidole vitano, vile vile na mguu. Vidole hivyo ni kama vifuatavyo:

-Gumba: Kidole cha mkono au mguu kilicho kinene na kifupi kuliko vingine.

-Kidole au chanda cha shahada : Kidole kinachofuata kidole gumba.

-Kidole au chanda cha kati: Kidole kinachofuata kidole cha shahada.

-Kidole au chanda cha pete: Kidole kinachopatikana kati ya kidole cha kati na cha mwisho.

-Kidole au chanda cha mwisho: Kidole kinachofuata kidole cha pete ambacho ni kidogo kuliko vingine.

Nafasi iliyoko katikati ya vidole huitwa **panda.**

Unaweza vile vile kupata sehemu za ndani ya mwili. Kwa mfano, kuna **kaakaa** ambalo ni sehemu ya juu ya kinywa. Kuna pia **ulimi** ambao ni kiungo cha mwili ndani ya kinywa kinachotumika kwa kuonjea, kusemea, kurambia, n.k. Halafu tena kuna meno mbalimbali kama **magego, meno ya mbwa, meno ya mbele** na **papachi.** Meno ya mbele hutumiwa kwa kukatia chakula. pia meno ya mbele yanaweza kuwa meno ya kwanza ya mtoto mchanga ambayo hung'oka yakatoka.

Meno ya mbwa ni meno yatumiwayo kwa kutafunia chakula. Meno haya huitwa hivi kwa sababu mbwa ana meno haya pekee. Lakini **magego** hutumiwa kwa kusagia chakula kinacholiwa.

Pengine, ndani ya mwili, kuna **moyo** ambao ni injini ya mwili. Halafu kuna **mapafu, ini, kongosho, tumbo, utumbo mdogo, utumbo mkubwa, wengu, kibofu** na **figo.**

Hali kadhalika, hizi ni baadhi tu ya sehemu za mwili wa binadamu, zipo nyingine ambazo hatukuzitaja na pia kumbuka kuwa si sehemu zote za mwili zilizo na majina katika Kiswahili.

4.10 MAGONJWA MBALI MBALI NA ILA ZA MWILI

Ugonjwa ni hali isababababishayo mtu kuwa katika afya mbaya. Lakini **ila** ni kasoro au hitilafu ya mwili labda kutokana na ugonjwa au kwa kuumbwa hivyo na Mwenyezi Mungu.

Ugonjwa upo namna kwa namna. Namna hizo ni kama vile **ukimwi, utanduu(utanuu), kidonda, kidonda ndugu, kikohozi, kidafuro, kichocho, kipindupindu, kuhara, kichomi, jipu(majipu), upele(pele), kusokota tumbo, kifafa, ukoma, homa, tauni, kiungulia, malaria, kupooza,** na nyingine.

Ukimwi ni neno linalotokana na ufupisho wa maneno: "**Upungufu wa Kinga Mwilini".** Ni ugonjwa unaotokana hasa hasa na zinaa(uasherati) na husababisha ukosefu ya kinga mwilini; yaani ni ugonjwa wa kuambukizwa kupitia njia ya ngono au vifaa vingine vinavyoweza kujeruhi mwili na kumwagia damu.

Utanuu ni ugonjwa wa utando ufunikao ubongo. **Kidonda** ni mahali mwilini palipokatwa ama kujeruhiwa na pakaugua. Mahali hapo pakiwa pakubwa huitwa **donda,** na pakiwa hapasikii dawa huitwa **kidonda ndugu.**

Kikohozi ni ugonjwa wa kifua ambapo mtu hushikwa na kikohozi na kukohoa kwa muda mrefu. **Kidafuro** ni ugonjwa wa kuambukizwa wa kukohoa sana ukitoa sauti kama filimbi. Ugonjwa huu hasa huwashika watoto wadogo. Magonjwa mengine ni kama vile **kichocho** ambao ni uwele wa kukojoa damu usababishwao na vijidudu vikaavyo katika konokono kwenye maji baridi yaliyotuama. **Kipindupindu** au **waba** ni ugonjwa wa kuhara na kutapika ambapo mgonjwa hufa kwa kukosa maji mwilini. **Kuhara** ni hali ambapo mgonjwa huenda choo cha maji maji. **Kichomi** ni maumivu kama kwamba kitu kikali chenye ncha kinachoma mbavuni ama kifuani. **Jipu** ni uvimbe mkubwa kwenye mwili na hutuga usaha. **Upele(pele)** ni vijipu vidogo sana vinavyotunga usaha. Kwa kawaida pele huwa nyingi mwilini. **Kusokotwa na tumbo** ni kuumwa na tumbo au kuumia tumboni. **Kaswende (sekeneko** au **farangi)** ni ugonjwa unaoshika uke au uume na huambukizwa kwa njia ya kujamiiana. **Kisonono** ni ugonjwa wa zinaa wa kuambukiza wa kutokwa na damu au usaha kwenye tupu ya mbele kisalisali. **Kifafa** ni ugojwa umfanyao mtu kuanguka na kupoteza fahamu kwa muda akipigapiga mikono na miguu na kutoa povu kinywani. **Ukoma** au **jedhamu** ni ugonjwa wa kuambukiza mabatomabato ambao unaharibu mishipa ya fahamu na kukata viungo vya mwili. **Homa** ni ugonjwa ambao unafanya joto la mwili kuwa juu zaidi kuliko kawaida. **Tauni** ugonjwa wa homa kali unaoambukizwa na viroboto vya panya. **Kiungulia** hali ya kuhisi kuchomeka kwenye umio na njia ya chakula juu ya tumbo kunakosababishwa na ongezeko la asidi tumboni. **Malaria** ni ugonjwa unaoambatana na homa ambao huletwa na mbu aitwaye anofelesi. **Kupooza** ni kupunguka au kukosa nguvu za kawaida. **Mbalanga** au **barasi** ni ugonjwa unaobadilisharangi ya ngozi na kuwa na mabaka au vitone. **Kisukari** ni ugonjwa unaosababishwa na kuzidi kwa sukari kuliko inayohitajika mwilini. **Kichaa** ni ugonjwa wenye upungufu wa akili au ugonjwa wa kujiwa na wazimu, ama kuwa mwendawazimu.

Kwa upande mwingine, zipo ila za mwili. Ila hizo zaweza kuwa kama vile **chongo, kipofu, kiziwi, bubu, kibyongo, kigugumizi, kengeza, kiguu, kiwete, kikono, mbilikimo, king'ong'o,** na nyingine.

Chongo ni mtu au hali ya kuwa na jicho moja lisiloona. Lakini **kipofu** mtu asiyeona kwa kupofuka kwa ajili ya kuugua ama kuzaliwa hivyo. Naye **kiziwi** au **kiduko** ni mtu asiyeweza kusikia. Lakini **bubu** ni mtu asiyeweza kusema. Mara nyingi chanzo cha ububu ni uziwi. **Kibiongo**(kibyongo,kiduva,kijongo,kigongo) ni mtu aliyepindika mgongo, au sehemu ya mgongo wa mtu yenye kinundu. **Kigugumizi** au **kitata** ni msemaji anayezungumza kama kuwa kitu kimezuia maneno. **Kengeza** ni jicho lenye mboni isiyokuwa katikati bali iliyokwenda upande. **Kiguu** au **kiguru** ni mtu ambaye mguu wake mmoja ni wenye kilema kama vile kupinduka. Lakini **kiwete** ni mtu mwenye kulemaa miguu yote miwili. Naye **kikono** ni mtu mwenye kilema cha mkono. **Mbilimiko (kibete** au **kibirikizi)** ni mtu aliye mfupi sana kuliko ilivyo kawaida. Kisha **King'ong'o** ni hali ya kusemea puani.

4.11 WANYAMA WAFUGWAO NA WANYAMA WASIOFUGWA

Kwa ujumla wanyama ni viumbe vyenye uhai, hasa hasa vyenye miguu mine, visivyokuwa watu, mimea au wadudu.

Kuna aina tofauti za wanyama, wanyama hao ni kama wanyama wafugwao, yaani wanyama wa nyumbani. Kuna pia wanyama wasiofugwa, yaani wanyama waporini.

WANYAMA WA KUFUGWA (WANYAMA HOWA)

Katika wanyama wafugwao, hebu tuangalie baadhi ya wanyama hao :

1. Ng'ombe : ni mnyama wa jamii ya nyati anayefugwa na hutumiwa kupata nyama, maziwa na ngozi. Pia na kwato zake hutumiwa kutengenezea gundi.

2. Mbuzi : Ni mnyama anayefanana na swala, anayefugwa kwa ajili ya kutoa nyama au maziwa.

3. Mbwa : Mnyama afugwaye ambaye husaidia watu kuwinda na kulinda.

4. Nguruwe : Ni mnyama afugwaye aliye mnene na mfupi, mwenye pua kubwa na ndefu, miguu mifupi, mkia mfupi na ambaye waislamu huamini kuwa ni haramu.

5. Kondoo : Mnyama afugwaye mkubwa kama mbuzi mwenye manyoya marefu yatengenezwayo sufu na kutoa mavazi(nguo) ya kuvalia. Anaweza pia kuitwa Ng'onzi.

6. Sungura : Mnyama mdogo mwenye masikio marefu na mkia mfupi. Yaweza pia kuitwa Kitungule.

7. Paka : Ni mnyama mdogo wa jamii ya chui anayefugwa nyumbani na anayependa kula panya.

8. **Panya :** Ni mnyama kama buku mdogo mwenye pua iliyochongoka, mkia mrefu na masharubu, paka humpenda sana kama chakula chake.

9. Punda : Mnyama wa jamii ya farasi mwenye miguu mifupi na mdogo zaidi kuliko farasi na hutumiwa zaidi kwa kukokota magari au kubeba mizigo.

10. Farasi : Ni mnyama wa kufugwa wa jamii ya punda lakini mkubwa zaidi kuliko punda, mwenye singa shingoni na mkiani na hutumika kubeba watu, mizigo na kuvuta gari au kwenye michezo ya kukimbia.

11. Ngamia : Ni mnyama mkubwa kama Twiga mwenye nundu ambaye hutumika katika safari za jangwani.

WANYAMA WA PORINI (WANYAMA WASIOFUGWA)

Wanyama wa porini au wanyama wasiofugwa nyumbani, ni wanyama wengi sana na hatuwezi kuwazungumzia wote, bali tutapitia chache tu.

1. **Chui:** Ni mnyama wa msituni(mwituni) wa jamii ya paka lakini mkubwa na mkali mwenye madoadoa ya njano na meusi.

2. **Duma:** Ni mnyama mkubwa wa porini mwenye umbo kama la paka na chui.

3. **Simba:** Ni mnyama mkubwa wa poirini wa jamii ya paka mwenye manyoya ya rangi majani makavu na ambaye hula nyama.

4. **Nyati au mbogo:** Ni mnyama wa porini mkubwa mithili ya ng'ombe mwenye pembe zilizopinda kwa mbele.

5. **Tembo au Ndovu:** Ni mnyama mkubwa sana wa porini mwenye mkonga na pembe mbili kubwa zenye thamani kubwa sana.

6. **Pundamilia:** Ni aina ya mnyama wa porini wa jamii ya farasi mwenye miraba myeusi na myeupe mwili mzima.

7. **Twiga:** Ni mnyama mrefu sana wa rangi ya kahawia na mabatomabato meusi na ndefu anayepatikana katika bara la Afrika.

8. **Sokwe au sokwemtu: N**i mnyama wa jamii ya nyani asiyekuwa na mkia.

9. **Nyani:** Mnyama anayefanana na tumbiri lakini mkubwa zaidi mwenye rangi ya kaki ya kijivu na ngoko(doa) nyekundu matakoni.

10. **Tumbiri au tumbili:** Ni mnyama mdogo wa jamii ya nyani, mwenye rangi ya kijivu na nyeupe tumboni, miguuni kifuani, mwenye mkia mrefu na uso mweusi.

11. **Ngedere:** Ni mnyama mdogo wa jamii ya nyani na tumbiri.

12. **Kifaru:** Ni mnyama mkubwa afananaye na kiboko na mwenye kipusa usoni.

13. **Buku: Ni** panya mkubwa na mwenye mkia mrefu kama ndezi.

14. **Ndezi:** Mnyama wa mwituni mwenye umbo kama la panya na mkubwa kuliko panya.

15. **Nungu au nungunungu:** Aina ya mnyama mdogo anayefanana na nguruwe kwa sura, mwenye miba mwili mzima iliyo kama vijiti vyembamba vilivyochongoka.

16. **Mjusi:** Ni mnyama wa jamii yenye damu baridi, mdogo kuliko kenge, huishi mashimoni au miambani. Anaweza pia kuitwa lumbwi.

17. **Kinyonga:** Mjusi anayebadirika rangi ya mwili wake ili ifanane na rangi ya mazingira alimo.

18. **Kobe:** Ni mnyama mwenye gamba gumu, shingo fupi na aendaye polepole.

19. **Mbwamwitu:** Mnyama wa jamii ya mbwa aishiye porini.

20. **Mbweha au bweha: N**i mnyama anayefanana na mbwamwitu lakini mdogo kidogo mwenye masikio marefu yaliyosimama, mdomo mrefu mwembamba na hukamata sana kuku.

21. **Paa:** Ni mnyama wa porini aliyefanana na mbuzi, mwembamba na mdogo, mwenye rangi ya kijivu na hudhurungi mgongoni, nyeupe tumboni, pembe ndefun na mkia wa kahawia na weupe nchani.

22. **Swala au swara:** Ni mnyama wa jamii ya kurungu na tohe afananaye na mbuzi mkubwa.

23. **Tohe:** Mnyama wa jamii ya kurungu na paa.

24. **Fisi:** Ni mnyama wa mwituni mwenye ukubwa kama wa beberu, ana rangi ya kijivu na anayeaminiwa kuwa ni mwoga na anayependa kula sana mizoga. Yaweza pia kuitwa Bakaya.

25. **Nyoka:** Ni mnyama mrefu na mwembamba mwenye magamba na asiye na miguu, anayetambaa na kutaga mayai. Huwa na sumu, hula wadudu na vinyama vidogovidogo.

    Mfano : Kuna nyoka aitwaye Chatu, Swila au Fira, Mamba, Bafe au Moma, n.k.

    Chatu ni nyoka mkubwa na mnene anayeua kwa kujivingirisha mwili wa windo lake.

    Swila au Fira ni nyoka mwenye mate yenye sumu na ambaye huvimbisha shingo wakati wa kurusha mate yake.

    Mamba ni nyoka mweusi au wa kijani mwenye sumu kali sana.

    Bafe au Moma ni aina ya nyoka mwenye mate yenye sumu.

26. **Kicheche au cheche :** Ni mnyama kama paka mwitu ambaye hukamata kuku.

WANYAMA WA MAJINI

Wanyama wa majini nao wako katika aina mbalimbali. Miongoni mwa wanyama hao tunaweza kutoa mifano k.v. **samaki** amabaye ni kiumbe kinachoishi ndani ya maji k.v. baharini, ziwani au mtoni, chenye mapezi na mkia ambavyo ndivyo viungo vinavyomwezesha kwenda au kupumua kwa kutumia mashavu.

Wanyama hawa nao wako katika aina nyingi sana k.v. **Papa** ambaye ni samaki mkubwa wa baharini asiye na mamba mwenye ngozi nene ya kijivu.

Kuna pia **pomboo** ambaye ni samaki mkubwa wa baharini anayefanana na papa na asiye na mamba mwenye rangi ya kijivu iliyochanganyika na hudhurungi na hudaiwa kuwa hufuata vyombo vya kusafiria.

Kuna **dagaa** ambao ni samaki wadogowadogo. Naye **kambare** ni samaki wa mtoni au ziwani mwenye masharubu.

Isipokuwa aina za samaki ambazo ni nyingi, kuna pia na wnyama wengine wanaoishi majini k.v. **Chura** ambaye ni mnyama mdogo mwenye ngozi laini asiye na mkia ambaye anarukaruka sana akaaye katika nchi kavu na katika maji.

Kiboko naye ni mnyama mkubwa na mnene anayeishi katika maji baridi. **Mamba** naye ni mnyama mkubwa mwenye magamba akaaye mtoni na ziwani.

Hakika, wanyama wanaoishi majini ni wengi chungu nzima, na huu ulikuwa mdokezo tu.

NDEGE WA KUFUGWA (WA NYUMBANI)

1. **Kuku:** Ni ndege anayefugwa na anayefanana sana na kware mkubwa mwenye kutaga mayai.

2. **Jogoo: N**i kuku dume. Yaweza pia kuitwa jimbi au kikwara.

3. **Njiwa:** Ni ndege mkubwa kuliko tetere na mwenye raangi ya kijivu au weupe usiokoza na ambaye hula nafaka. Yaweza pia kuitwa hua au hamamu.

4. **Bata:** Huyu ni ndege anayeweza kufugwa au akawa wa porini, ni mkubwa kuliko kuku na hupenda kukaa majini, mwenye miguu mifupi yenye utando wa ngozi katikati ya vidole unaomwezesha kuogelea majini.

5. **Batamzinga:** Ni ndege mkubwa afananaye na bata mwenye manyoya ya kahawia, kichwa kisicho na manyoya, na shingo yenye ngozi ya makunyanzi isiyo na manyoya.

6. **Kasuku:** Ni ndege mkubwa mwenye rangi nyingi anayeweza kuiga kusema kama binadamu na mara nyingi hufugwa katika nyumba.

NDEGE WA PORINI

1. Bundi au bumu: Ni ndege mkubwa arukaye usiku tu na mwenye macho makubwa yanayomwezesha kuona gizani, hudhaniwa kuwa ni ndege mwenye kuleta kisirani au msiba. Yaweza pia kuitwa Babewana au Babewatoto.

2. Kanga: Ni ndege wa jamii ya kuku anayeishi porini, mwenye rangi ya kijivu iliyokoza na madoadoa meupe.

3. Tausi: Ndege mkubwa mwenye madoa ya rangi mbalimbali, k.v. buluu na kijani, ambapo dume lina mkia mpana na mrefu ambao huuchanua na kuufunga.

4. Popo: Ni mnyama mdogo kipofu mwenye mbawa anayefanana na panya, hupenda kula matunda na wadudu na kuruka usiku.

5. Chiriku: Ni ndege mdogo mwenye kelele sana.

6. Mbayuwayu: Ni ndege mdogo mwenye rangi nyeusi na nyeupe kooni na mgongoni karibu na mkia, ana mkia mrefu mwenye panda(mgawanyiko) na mbawa zilizokaa kama upinde arukapo na hujenga kiota cha manyoya na udongo.

7. Mwewe: Ndege mkubwa anayefanana na tai ambaye hukamata vifaranga vya kuku.

8. Tai: Ni ndege mkubwa mwenye kucha ndefu na kali ambaye chakula chake kikuu ni mizoga.

9. Kunguru: Ndege mkubwa mweusi au mwenye baka jeupe shingoni.

10. Flamingo au heroe: Ni ndege mwenye miguu mirefu nyekundu, shingo ndefu na mwili wa rangi nyeupe, hupatikana kwenye maziwa.

11. Korongo: Ndege mwenye shingo ndefu na miguu mirefu, mwenye kujivuna na kujinyonga kwa uzuri wake.

12. Mbuni: Ni ndege mkubwa wa mbugani asiyeweza kuruka lakini anayekwenda mbio sana kwa miguu yake.

WADUDU

Wadudu ni viumbe vidogo vyenye mbawa nne, miguu mingi na bila ya uti wa umugongo k.v. mbu, mchwa au mende.

Wadudu wako katika aina tofauti, hebu tuangalie mifano michache.

1. **Mbu:** Huyu ni mdudu mdogo mwembamba anayefyonza damu na huweza kuambukiza maradhi k.v. malaria, matende au homa.
2. **Kupe:** mdudu mdogo ambaye huganda kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu na huambukiza magonjwa.
3. **Kiroboto:** Ni mdudu mdogo sana anayeuma na kufyonza damu na hupenda kukaa katika vumbi, katika manyoya ya paka au ya mbwa.
4. **Nzi:** Ni mdudu mwenye mbawa nne na hupatikana mahali penye uchafu au kinyesi na hueneza magonjwa.

5. **Nzige:** Mdudu aina ya panzi lakini mkubwa na anayesafiri masafa marefu **kwa makundi na huharibu mimea.**

6. **Kipepeo:** Mdudu mwenye umbo jembamba na mbawa pana zenye rangi mbalimbali na hupendelea kwenye maua.

7. **Panzi:** Ni mdudu wa jamii ya nzige, mwenye umbo refu, meno meusi mawili, mbawa nne na miguu sita ambayo miwili miongoni mwake ni mikubwa zaidi na hutumika kwa kurukia na kujihami.

8. **Nge(scorpion):** Ni mdudu wa rangi ya kahawia au nyeusi mwenye miguu minane na mkia mrefu wenye mwiba wa sumu nchani(mwishoni).

9. **Chawa:** Ni mdudu mdogo akaaye mwa mwanadamu, hasa katika nywele na nguo chafu na humnyonya damu.

10. **Mchwa:** Mdudu mweupe wa jamii ya chungu anayejenga kichuguu na hula sana miti na vitu vilivyotengenezwa kwa miti.

11. **Nyigu:** Ni mdudu wa jamii moja ya nyuki anayeuma, na mwenye kiuno chembamba. Mdudu huyu yaweza pia kuitwa dondora au mavu.

12. **Nyuki:** Mdudu mwenye mbawa nne anayeweza kuuma, anayeishi katika kikundi kwenye mzinga na hutengeneza asali na nta.

13. **Kombamwiko au mende:** Ni mdudu wa rangi ya kahawia mwenye mbawa nne na miguu sita, anayependa kutafuna vitu k.v. karatasi, kitambaa au nafaka na apendaye kukaa sehemu za giza.

14. **Jongoo:** Mdudu mweusi au wa kahawia mwenye miguu mingi sana.

15. Sisimizi: Mdudu mdogo wa kahawia au mweusi mwenye umbo na sura kama siafu. Yaweza pia kuitwa nyenyere au chungu.

16. **Siafu:** Ni mdudu mdogo wa jamii ya chungu anayekwenda pamoja na kundi la wenzake, mwenye rangi ya kahawia na ambaye anauma sana.

17. **Kunguni:** Mdudu mdogo anayefyonza damu, ambaye hukaa kwenye vitanda.

18. **Buibui:** Ni mdudu mwenye miguu minane myembamba atandazaye utando wa kukamatia nzi na wadudu wengine.